
epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com | www.ippmedia.com | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Oktoba 24, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
# Nipashe
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581839
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

# CHADEMA yaguna




• **CCM** yasema itakubali matokeo yoyote... *Endelea ukurasa wa 2 & 8*

UKURASA WA 3

**MAKAMU WA RAIS AITA WAWEKEZAJI NISHATI JOTOARDHI**



UKURASA WA 4

**NMB, UDSM WAKUBALIANA KUWAWEZESHA WANAFUNZI WABUNIFU**



UKURASA WA 5

**TCRA YAJIGAMBA KUMALIZA LAINI ZA 'TUMA NAMBA HII'**



UKURASA WA 7

**MWINYI AAHIDI FEDHA ZAIDI SEKTA YA ELIMU**



Majeneza yaliyobeba miili ya wanakwaya watano wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Usharika wa Tegeta waliofariki katika ajali iliyotokea eneo la Kirinjiko yakiwa katika kanisa la KKKT Tegeta, Dar es Salaam jana kwa ajili ya ibada ya kuaga. **PICHA: EATV**

## Wanaoishi na selimundu wataka upimaji kabla ya ndoa

UKURASA 5

# Simanzi miili wanakwaya watano KKKT ikiagwa

UKURASA 3

**MICHEZO** GAMONDI ATAMBIA UBORA WA YANGA UK.24 **KATUNI** UK.6

# TACAIDS iongeze kasi huduma VVU/UKIMWI jamii za wavuvi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI imeagiza Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kuongeza kasi ya utoaji elimu ya kujikinga na Virusi vya UKIMWI (VVU), huduma za kinga, matibabu na matunzo miongoni mwa wavuvi katika maziwa na bahari.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Dk. Christina Mzava pamoja na kamati yake walisema juzi jijini hapa kuwa elimu ya kujikinga na VVU miongoni mwa jamii ya wavuvi ipo chini, hali kadhalika upatikanaji huduma za VVU na UKIMWI si wa kuridhisha.

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, wakijadili baada ya taarifa ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega kuwasilishwa kwa kamati hiyo kuhusu hatua za ujumuishaji afua za VVU na UKIMWI kwenye sekta ya uvuvi, walisema elimu ya kujikinga na VVU, pamoja na huduma za kinga, matibabu na matunzo miongoni mwa wavuvi bado zinahitaji kuongeza kasi kwa kuwa hali ya maambukizi kwa wavuvi bado ipo juu.

Kaimu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Christina Mzava, alisema TACAIDS ina kazi kubwa ya kufanya katika sehemu za mialo ili kuokoa jamii za wavuvi kutokana na kuwa na ushamiri wa juu wa VVU kwa kuwa asilimia saba ambayo ni zaidi ya kiwango cha kitaifa.

Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala, Samweli Mwashamba, akiwasilisha taarifa ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa niaba ya Waziri Ulega, alisema wizara na taasisi zake 10 inaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji afua za VVU, UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukizwa (MSY) mahala pa kazi kwa mujibu wa Waraka Na 2 wa Utumishi wa Umma wa Kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY Mahala pa Kazi katika Utumishi wa Umma wa Mwaka 2014.

Alitaja maeneo yanayotekelezwa na wizara hiyo kuwa ni pamoja na kujumuisha masuala ya uvuvi na UKIMWI katika Sera ya UVUVI ya Mwaka 2015, kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya utekelezaji masuala ya kudhibiti VVU na UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza, kutoa elimu lishe na upimaji wa hiari kwa watumishi pamoja na kaanzisha vituo vya upimaji na ushauri nasaha kwa wavuvi.

Pia aligusia kuunda Kamati ya VVU na UKIMWI na Magonjwa Yasiyoambukiza pamoja na kuwa na mratibu wa UKIMWI, usambazaji makasha ya kuhifadhi kondomu na kondomu katika maeneo ya kazi ya wizara.

Alitaja sababu zinazochangia jamii za wavuvi kuwa na maambukizi ya VVU ni pamoja na matumizi hafifu na yasiyo sahihi ya kondomu na imani mbovu za kutoamini kondomu kwamba zinaweza kutumika na kuleta furaha ya tendo.

Pia kuna uelewa mdogo juu ya elimu ya VVU na UKIMWI katika kambi za wavuvi ambao hupelekea kufanyika ngono zisizo salama pamoja na kutokuwa na tabia ya kupima afya zao mara kwa mara ili kuweza kuwa na ufahamu wa afya zao pamoja na upatikanaji hafifu wa huduma za VVU na UKIMWI katika maeneo ya mialo hasa visiwani.

Alisema kuwa wanafanya pia sensa za wavuvi ili kuweka mkakati wa namna ya kutoa huduma za upimaji na ushauri nasaha, huduma za VVU na UKIMWI zinazotolewa asilimia 51 katika mialo 1,307.

Samweli Mwashamba alifafanua kuwa jumla ya kondomu 334,872 na makasha 30 ya kuhifadhi kondomu yamesambazwa kwenye wizara na taasisi zake katika kipindi cha mwaka 2023/24. Lishe na nauli kwa watumishi wa wizara na taasisi ambao walijiweka wazi kuwa wanaishi na VVU katika kipindi cha mwaka 2023/24.

Watumishi 387 walipatiwa elimu ya juu ya VVU na UKIMWI na ushauri nasaha pamoja na kufanyiwa vipimo.




Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwa katika mkutano wa mawaziri wa fedha na magavana wa Benki Kuu za nchi za Afrika (African Caucus - WB) uliomshirikisha Rais wa Benki ya Dunia, Ajay Banga, jijini Washington D.C, Marekani jana. Waziri Nchemba, anaongoza ujumbe wa Tanzania katika Mikutano ya Mwaka ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia. **PICHA: BENNY MWAIPAJA**

# CHADEMA yaguna uandikishaji wapigakura wa Serikali za Mitaa

**Na Mussa Mwangoka,** MPANDA

UONGOZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) mkoani Katavi umekosoa uandikishaji wapigakura wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ukidai kuwa uligubikwa na dosari nyingi.

Umesema dosari hizo hazipaswi kujirudia katika hatua nyingine za mchakato wa uchaguzi huo kwa kuwa zinatia doa uchaguzi huo na mustakabali wa demokrasia nchini.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Katavi, Rhoda Kunchela, alitoa rai hiyo jana wakati akizungumzia mchakato wa uchaguzi huo uliopangwa kufanywa Novemba 27, mwaka huu.

"Kuna kasoro nyingi: Majina kuandikwa kwenye makaratasi ya kawaida, si kwenye daftari la Tume Huru ya Uchaguzi; wanafunzi wasio wakazi wa eneo husika kuandikishwa, pia watoto chini ya miaka 18 kuandikisha kupiga kura na mengine mengi ambayo tumeainisha na kuitaka Tume ya Uchaguzi ishughulikie ili isitie doa uchaguzi huo," alisema.

Hata hivyo, uchaguzi huo unasimamiwa na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) licha ya marekebisho ya kisheria kuelekeza usimamiwe na Tume Huru ya Uchaguzi (INEC).

Alisema hawategemei hatua zinazofuata kwenye mchakato huo ziwe na malalamiko, hivyo mamlaka inayousimamia itende haki kuanzia kwenye uchukuaji fomu na inapofika hatua ya mapingamizi, haki pia itendeke, vivyo hivyo wakati wa kampeni hadi siku ya upigaji kura.

> **"Kuna kasoro nyingi: Majina kuandikwa kwenye makaratasi ya kawaida, si kwenye daftari la Tume Huru ya Uchaguzi; wanafunzi wasio wakazi wa eneo husika...**

Rhoda ambaye amewahi kuwa mbunge wa viti maalumu mkoa huo, alisema CHADEMA imewashawishi wananchi kujitokeza kujiandikisha kwa kuwa wengi wao walionesha kukata tamaa kutokana na kila mara kuporwa haki yao.

Hivyo, wana matumaini uchaguzi huo utatoa taswira ya nini wanatakiwa kufanya kwenye Uchaguzi Mkuu ujao wa rais, wabunge na madiwani.

Kwa mujibu wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mohamed Nchengerwa, wananchi waliojiandikisha kupiga kura kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Novemba 27, mwaka huu mkoani Katavi ni asilimia 96.37 ya waliotarajiwa kuandikishwa katika mkoa huo.

Oktoba 21 mwaka huu, wakati akifunga uandikishaji wapigakura kwa ajili ya uchaguzi huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, alivitaka vyombo vya dola nchini kuhakikisha vinaimarisha usalama ili uchaguzi huo uwe wa huru na haki.

Alipoulizwa kuhusu malalamiko ya vyama vya siasa, ikiwamo CHADEMA, kwamba baadhi ya wanafunzi wameandikishwa kupiga kura, Waziri Mchengerwa alisema, hoja hiyo haina mashiko "kwa sababu katika shule wapo pia wanafunzi waliozidi umri wa miaka 18 ambao sifa zinawaruhusu kupiga kura".

Alipoulizwa kuhusu malalamiko ya CHADEMA na ACT Wazalendo kuhusu eneo la Mirerani, mkoani Manyara kwamba uandikishaji ulifanyika hadi usiku, waziri huyo alisema "sina malalamiko hayo na sifahamu chochote. Kama tungepata taarifa hiyo, tungeifanyia kazi, tunataka uchaguzi wa huru na wa haki."

Kwa mujibu wa Waziri Mchengerwa, jumla ya wapigakura 31,282,331 wameandikisha kwa ajili ya uchaguzi huo sawa na asilimia 94.83 ya lengo la kuandikisha watu 32,897,8579.

**Soma zaidi Uk. 8**

**Kwa maoni: +255 677 020 701**
**Email: customerrelations@guardian.co.tz**

HABARI KITAIFA

# Makamu wa Rais aita wawekezaji jotoardhi

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI imetoa wito kwa wawekezaji kutoka nchi mbalimbali kuwekeza nchini kwenye sekta ya nishati hususan jotoardhi inayozalisha umeme na kusaidia kuondoa matumizi ya nishati chafu.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alitoa wito huo jana alipozindua Kongamano la 10 la Jotoardhi la siku tatu linalofanyika Dar es Salaam kwa siku tatu, ikiwa ni mara ya pili kufanyika nchini.

Dk. Mpango alisema nguvu ya ziada kutoka kwa wawekezaji inahitajika ili kufanikisha upatikanaji wa rasilimali hiyo muhimu na kwamba serikali ikiachiwa peke yake itakuwa na ucheleweshaji wa upatikanaji wa nishati hiyo.

Alisema serikali imeweka mazingira mazuri ikiwamo sera nzuri sambamba kuwapo kwa uchumi unaokua kwa asilimia tano hata baada ya ugonjwa wa UVIKO- 19.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, alisema jotoardhi ina uwezo mkubwa kama rasilimali maalum kwa eneo na ikitumika na kuunganishwa katika gridi ya taifa, manufaa yake yanaweza kusambazwa kwa usawa, kusaidia kukabiliana na tofauti za kijiografia katika upatikanaji wa nishati ambazo zinaakisi tofauti kubwa za kiuchumi.

"Katika usambazaji wa nishati ulio sawa, jotoardhi ina jukumu muhimu katika kushughulikia vipimo vya kijiografia vya ukuaji, ikiwaruhusu raia wengi zaidi kushiriki na kufaidika na maendeleo ya taifa," alisema.

Kapinga alisema kutokana na umuhimu wa rasilimali hiyo, ana uhakika kwamba mkutano huo utajadili na kulipatia suluhisho la kuondokana na mambo yanayozuia maendeleo ya jotoardhi.

Naye Mbunge wa Mbozi, George Mwenisongole, akiwawakilisha wabunge wanaotoka kwenye mikoa yenye rasilimali ya jotoardhi kuwa wananchi wanaoishi kwenye maeneo yenye miradi husika watapewa kipaumbele cha kupewa umeme.

Mbunge wa Igunga, Nicholas Ngasa, alisema juhudi za serikali zinatoa tumaini kwa kuwa inaonyesha nia ya wazi ya kuwaletea wananchi maendeleo kwa kukomesha adha ya kukatika umeme.

Vyanzo vya joto ardhi Tanzania ni 52 vinavyopatikana katika mikoa 16, vikitajwa kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme usiopungua Mw 5,000.

Wizara ya Nishati kwa sasa imejikita katika kutekeleza miradi mitano ya kipaumbele ambayo ni Ngozi (MW 70), Kiejo-Mbaka (MW60), mkoani Mbeya na Songwe (MW5), Luhoi (MW5) Pwani na Natron (MW60) Arusha.



Watoto wakiwa katika mafunzo ya kuandaa mabaki ya matunda kwa ajili ya kutengeneza mbolea, ambayo yalitolewa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIAKA**

# Simanzi miili wanakwaya KKKT ikiagwa

**Na Halfani Chusi**

VILIO, simanzi vimetawala wakati wa kuaga miili ya wanakwaya watano wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Wazo, Dar es Salaam, waliofariki dunia juzi katika ajali ya gari, eneo la Kirinjiko, Same, mkoani Kilimanjaro.

Wanakwaya hao walifariki dunia wakati wakienda kumzika mwanakwaya mwenzao, Machame, wilayani Hai, Kilimanjaro aliyefariki siku nne zilizopita wakati akijifungua.

Wanakwaya hao ni Stephen Temba, Auleria Swai, Neema Ngusi, Charles Mchome na Maderina Mtenzo. Mbali na wanakwaya hao walipoteza maisha, wengine walijeruhiwa na kupelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Same, Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mawenzi na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC.

Ibada ya kuaga miili ya wanakwaya hao iliongozwa na Mkuu wa KKKT na Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP) Dk. Alex Malasusa, akisaidiwa na wakuu wa majimbo na wa dayosisi hiyo. Pia viongozi hao waliwaombea majeruhi wanaoendelea kupatiwa matibabu.

Akizungumza wakati wa ibada hiyo, Askofu Dk. Malasusa alisema wamepokea kwa mshtuko tukio hilo la kusikitisha huku wakipokea pia salamu za pole mbalimbali kutoka kwa maaskofu, viongozi wa dini, serikali na watu binafsi.

"Jana tulipofika katika ibada tulisema tumegundua Mungu wetu si wa kawaida. Mungu akiamua jambo haliwezi kuzuilika. Tunapopanga mipango ya kuishi, tujipatie moyo wa hekima na hekima ni kumjua Mungu na kuamini yupo.

"Msiba huu utupe moyo wa hekima. Wanadamu wengi tunahangaika na kuwaelimisha watoto ili wafanye vizuri katika masomo lakini tunasahau kumwomba Mungu awape watoto wetu mioyo ya hekima.

"Kuishi maisha ya ibada lakini ninamwomba Mungu atupe moyo wa hekima kama Daudi anavyotwambia Mungu atujulishe kuzihesabu siku zetu tupate moyo wa hekima. Basi tujibwage kwa Yesu kwa kuwa hatujui siku wala saa atakayotuita," alisema.

**"Jana tulipofika katika ibada tulisema tumegundua Mungu wetu si wa kawaida. Mungu akiamua jambo haliwezi kuzuilika. Tunapopanga mipango ya kuishi, ...**

Katika ibada hiyo, aliwasifu wanakwaya hao walifariki dunia kwa kupenda ibada na kwamba ni washindi mbele ya Mungu na walifanya kazi nzuri ya kumtukuza kupitia uimbaji.

Wasemaji wa familia kwa pamoja waliwashukuru watu mbalimbali waliowakimbilia katika kipindi chote cha msiba pamoja na kanisa kwa kuendesha ibada ya kuwaaga ndugu zao.

Familia ya Madelini Mtenzi ilisema: "Tunatoka shukrani kwa kanisa la Usharika wa Wazo, madaktari wa Same waliopokea miili ya ndugu zetu na majeruhi wengine. Mungu awabariki."

Msemaji wa familia ya Aurelia Swai, alilishukuru kanisa hilo huku akisema mpendwa wao watamsafirisha kumpeleka Moshi kwa ajili ya maziko yatakayofanyika keshokutwa.

Naye msemaji wa familia ya Neema Ngusi alisema hana maeneno mengi zaidi ya kumshukuru Mungu kwa kilichotokea.

Msemaji wa familia ya Stephen Temba aliushukuru uongozi wa kanisa hilo kwa kuwakimbilia katika msiba huo.

"Tunashukuru wote mliofika hapa kutuunga mkono. Mmeacha familia zenu asanteni sana. Familia ya Temba tunatoa shukrani hata kwa Mchungaji Kiongozi wa Usharika (wa Wazo, Herman Kiporoza). Mungu ampe moyo huo hata kwa matukio mengine. Pia tunawashukuru ndugu, jamaa na marafiki wote kwa kutukimbilia," alisema.

**Kwa maoni: +255 677 020 701**
**Email: customerrelations@guardian.co.tz**

# NMB, UDSM waingia makubaliano kuwawezesha wanafunzi wabunifu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) wametia saini mkataba wa makubaliano ya ushirikiano, unaolenga kukuza vipaji, ubunifu, uwekezaji katika mageuzi ya kidigitali na msaada wa kifedha kwa wanafunzi wa Chuo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Co-ICT) kilichoko chini ya chuo hicho.

Makubaliano hayo ya miaka mitano yalitiwa saini jana Makao Makuu ya NMB jijini Dar es Salaam, UDSM ikiwakilishwa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Utafiti, Prof. Nelson Boniface huku NMB ikiwakilishwa na Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu, Emmanuel Akonaay.

Akizungumza kabla ya kutia saini mkataba huo, Akonaay alisema NMB ambayo elimu ni sekta ya kipaumbele, inaamini kuwa makubaliano hayo yanakwenda kuchochea ubunifu miongoni mwa wanafunzi wa Co-ICT ambao utawezesha utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazozungukia jamii na taifa kwa ujumla.

Alibainisha ya kwamba makubaliano hayo yatajikita katika maeneo matano ambayo ni: Ukuzaji vipaji na ujuzi; ukuzaji ubunifu wa matumizi ya teknolojia; uwekezaji katika mageuzi ya kidigitali; utafiti wa teknolojia na maarifa; pamoja na msaada wa kifedha wa masomo kusaidia programu bunifu.

“Katika ukuzaji wa vipaji na ujuzi, kwa pamoja NMB na Co-ICT tutashirikiana katika kutambua na kuendeleza kupitia mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika nyanja za TEHAMA, kama itakavyokuwa kwenye ukuzaji wa ubunifu wa matumizi ya teknolojia.

“Hapo tutasaidia kuendeleza ushindani katika sekta ya fedha ambayo inakua kwa kasi sana, pande zote zitashirikiana katika kutoa fursa kwa wanafunzi kujaribu teknolojia tofauti zinazoweza kuwa na athari chanya kwa sekta ya kifedha kupitia SANDBOX,” alifafanua Akonaay.

Aliongeza kuwa katika mageuzi ya kidigitali, NMB na Co-ICT kwa pamoja watawekeza katika nyanja hiyo ili kuongeza ufanisi, kupunguza gharama na kuboresha huduma kwa wateja na katika utafiti wa teknolojia na maarifa, watashirikiana kufanya utafiti wa kiteknolojia ili kuchunguza athari zake kwa sekta ya fedha.

“NMB tunaamini makubaliano haya si tu yatasiadia kuimarisha mahusiano yetu, bali ni mwendelezo wa ushirikiano endelevu baina yetu na ahadi yetu ni kuwa NMB itaendelea kufanya kazi na serikali yetu katika sekta ya elimu, ambayo ni utekelezaji wa dhati wa dhamira yetu ya kuchangia ukuaji na ustawi wa elimu nchini.

“Tunashukuru UDSM Co-ICT kwa kuichagua NMB na kukubaliana kushirikiana katika kufanikisha matakwa ya kimkataba,” alisema Akonaay aliyemwakilisha Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna.

Mbali na makubaliano hayo, mchango na ushirikiano mwingine baina ya NMB na UDSM ni mkataba wa miaka miwili na Shule Kuu ya Biashara ya UDSM, ambako kwa miaka miwili benki imetumia Sh. milioni 35 kuwazawadia wanafunzi watatu bora waliofanya vizuri zaidi katika masomo ya biashara.

“NMB pia tumekuwa tukiandaa Career Fairs, ambayo tumeyatumia kuwakutanisha mamia ya wanafunzi, si tu kuwaonesha aina ya huduma zetu, bali kuwafunza namna ya kuomba kazi na kuwajengea uelewa wanafunzi wanaojiandaa kuingia katika soko la ajira, kuwajuza changamoto na mahitaji ya soko.

> **“Hali hii husababisha maji ambayo tunavuna ndani ya Ziwa Victoria kuwa na tope jingi na kutumia gharama kubwa ya dawa za kutibu maji. Kwa mwezi tunatumia kati ya Sh. milioni 300 hadi 350 kwa mwezi,” alisema Zengo.**

“Lakini pia kupitia NMB Foundation, tumekuwa tukitoa ufadhili wa NMB Nuru Yangu Scholarship and Mentorship, ambapo hadi sasa tuna wanafunzi 132, wako katika vyuo mbalimbali vya umma, ambako wametengewa Sh. bilioni 1.4 ili kuwawezesha kupata masomo yao hasa watokao mazingira magumu,” alisema.

Akonaay alisema benki yake imekuwa pia ikitoa programu ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi, ambapo jumla ya wanafunzi 1,500 waliomaliza vyuo vikuu wamekuwa wakifanya mafunzo hayo, wengi wao wakiwa wamechukuliwa na NMB na wengine wameajiriwa kwingineko.

Kwa upande wake, Profesa Nelson alishukuru NMB kwa kukubali kuingia mkataba wa makubaliano hayo, yanayompa uhakika kwamba yanakwenda kuwawezesha vijana wazuri wa ubunifu ambao watanufaika vya kutosha kupitia makubaliano hayo, yanayokwenda pia kuchachua teknolojia ya Akili Mnemba (AI).

“Tulikupokuwa tunateta kwamba, AI itakuwa ni sehemu ya mambo ambayo yatatekelezwa kupitia makubaliano haya, lakini je, AI tulizonazo zinajua kuongea lugha zetu tunapofanya biashara? Sasa hiyo ni changamoto ambayo tunapaswa kuitafutia ufumbuzi kwenye muundo wa kibiashara uliomo katika mkataba huu.

“Hii maana yake ni kuwa itatulazimu tutapowaendea watu wasiojua Kiingereza, wasiojua Kiswahili, tuweze kuwafikia kwa lugha zao za asili ili kufanikisha malengo na mipango ya kibiashara. Nadhani hapo NMB itakuwa ‘giants’ wa ubunifu,” alisema Prof. Nelson.

Alisema UDSM na Co-ICT inao vijana wengi, wazuri na mahiri katika ubunifu, anaoamini kuwa wakati wao kunufaika na makubaliano hayo ni sasa na kuwataka NMB kuunga mkono harakati zao si tu ili kuwawezesha kuingia katika soko la ajira, bali pia kujiajiri itakapolazimika.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 5(1) ya Kanuni za Mafuta (Compressed Natural Gas) (Supply and Marketing Services Rules, GN No. 220 of 2019).**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kibali cha ujenzi wa kituo cha kujaza gesi asilia iliyoshindiliwa kwenye magari kutoka **PUMA ENERGY TANZANIA LIMITED** kitakacho jengwa kiwanja namba 1C/1 eneo la Mabibo katika Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam.

Hivyo, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha **EWURA** kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;
Namba ya Bure 0800110030;
Barua pepe: **info@ewura.go.tz** Tovuti: **http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 6(1&3) ya Kanuni za Mafuta, the Petroleum (Natural Gas)(Transmission and Distribution Activities), GN No. 176 of 2018).**

**TAARIFA**inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kibali cha ujenzi wa bomba la kusambazia gesi asilia kutoka Kisemvule, Mkuranga Pwani hadi Mbagala, Temeke, Dar es Salaam lenye urefu wa kilometa 18.2 kutoka kwa kampuni ya Rashal Energies Limited.

Hivyo, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;
Namba ya Bure 0800110030;
Barua pepe: **info@ewura.go.tz** Tovuti: **http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz

# Pinda achangisha milioni 130/- ujenzi kituo cha watoto yatima

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Mkazi, Geophrey Pinda, ameongoza harambee iliyochangisha Sh. milioni 132 kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa kituo cha watoto yatima cha The Joy of God Ophanage Center, jijini Arusha.

Hafla ya harambee hiyo ilifanyika juzi katika nyumba ya Bushback Safari Kilenge iliyoko mtaa wa Impla, jijini Arusha.

Akitoa shukurani kwa wananchi, wadau pamoja na viongozi wa serikali waliofika katika harambee hiyo, Pinda aliwaomba Watanzania kujitoa kuwasaidia, kuwalea na kuwajengea makazi watoto wasio na uwezo, wakiwamo yatima.

"Tutakuwa na ushahidi kwamba tuna kitu tutakifanya, hizi Sh. milioni 132 zinakwenda kusaidia watoto hawa wenye uhitaji maalumu.

"Uhitaji maalumu maana yake hawana walezi na sasa tumeamua kusaidiana na mtawa katika kuwalea, kuwajengea makazi na maisha yao kuwa salama," alisema Pinda.

Alishukuru taasisi zote za kifedha zilizoshiriki katika harambee hiyo huku akiomba taasisi nyingine zenye nafasi ya kuchangia ujenzi zaidi wa kituo hicho, kushiriki kusaidia watoto hao.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, aliwashukuru wananchi kwa kujitolea kwa moyo wa dhati katika kuhakikisha wanafanikisha ujenzi wa kituo hicho.

"Niwashukuru sana kwa namna mlivyoguswa katika utoaji wenu, hakika ni jambo la kushukuriwa mno ili kuwalea vyema watoto wetu hawa," alisema Mtahengerwa.

Mlezi wa kituo hicho, Sista Janeth Ngopa alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kupitia kwa Naibu Waziri wa Ardhi kwa kushiriki na kuendesha haramabee hiyo kikamilifu kufanikisha ujenzi wa kituo hicho.

"Kwa niaba ya watoto, wadhamini na bodi ya kituo hiki, ninamwomba Mungu ampe maisha marefu Mungu, ampe afya njema na tunamwomba asichoke kutusaidia kwa sababu mara kwa mara tutamsumbua kwa njia ya simu kutusaidia," alisema Sista Janeth.

Katika kuboresha makazi ya watoto hao wasio na uwezo, kituo hicho kimeanzisha na kinaendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa mbili ambalo msingi wake umekamilika katika eneo la Gomba Estate, jijini Arusha.

# TCRA kumaliza laini 'tuma kwa namba hii'

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema inaendelea kushughulikia laini za simu zinazotumika kufanya utapeli wa mtandao ili kuzimaliza kabisa.

Katika kufanya hivyo, TCRA imesisitiza kuwa kila ujumbe mfupi wa maneno 'sms' utakaotumwa utarekodiwa.

Akitoa wasilisho la Ripoti ya Tathmini ya Mawasiliano Tanzania inayoanzia Juni hadi Septemba, mwaka huu, Mkurugenzi wa Masuala ya Kisekta wa TCRA, Mhandisi Felician Mwesigwa, huku akiwanyoshea kidole mawakala wasio waaminifu wanaosajili laini kwa njia ambazo ni kinyume na utaratibu.

Ripoti hiyo ilionesha kuwa mikoa ya Rukwa na Morogoro imeongoza kwa kuwa na majaribio ya ulaghai wa kimtandao huku ikibainisha kuwa katika maeneo mengine matukio hayo yamepungua kwa asilimia 28, ikilinganishwa na yaliyoripotiwa katika ripoti ya Juni, mwaka huu.

"Mikoa hiyo imeongoza mwaka mzima. Kuna mtu anaamua kusajili laini ya simu ili akafanye kile anachoona ni fursa kwake. Mtu anajua kabisa kwamba nikifanya kosa kuna sheria zake lakini bado anafanya, hivyo kazi yetu sisi ni kuhakikisha upatikanaji wa laini hizo usiwe rahisi. "Watoa huduma wengi wametumia teknolojia za kubaini hizo 'sms' na kuzifungia laini husika pia kuwaangaliwa wale ambao wamesajili laini hizo zilizotumika kwenye kufanya matukio ya kitapeli. Hiyo inakwenda sambamba na hatua mbalimbali za udhibiti," alisema Mwesigwa.

Ripoti hiyo ambayo hutolewa na TCRA kila baada ya miezi mitatu, ilionesha kwamba mikoa hiyo imeongoza kwa kuwa na theluthi moja ya majaribio ya ulaghai kupitia simu za mkononi kwa kutumwa ujumbe mfupi wa maneno mfano 'hiyo fedha nitumie kwa namba hii 0713 46... jina litatoka ...).

Njia nyingine ya utapeli inayotumika katika maeneo hayo, ilielezwa kuwa ni tapeli kumpigia simu ya moja kwa moja mtu mwingine na kujitambulisha kuwa ni mtoa huduma wa mtandao fulani na kumpa maelekezo ambayo endapo mhusika atayafuata yatasababisha kutapeliwa.

Kutokana na hali hiyo mitandao mbalimbali ya laini za simu imekuwa ikitoa elimu na msisitizo kwa wateja kwamba watawasiliana nao kwa namba 100 pekee, hivyo wajiepushe na kufuata maelekezo yoyote watakayopatiwa na mtu aliyewapigia kwa namba binafsi.

"Kila mwaka kwenye ripoti zetu, mikoa ya Rukwa na Morogoro imekuwa na matukio mengi ya ulaghai. Wilaya zilizoongoza kwa Rukwa na matukio yake kwenye mabano ni Simbawanga (5,198), Nkasi (250) na Kalambo (122) huku Morogoro zikiwa ni Ifakara (3,922), Kilombero (1,306), Morogoro (127), Kilosa (89), Ulanga (21), Mvomero (10), Malinyi (manane) na Gairo (matatu).

Mhandisi Mwesigwa pia alitaja mikoa iliyofuatia kwa matukio ya majaribio ya utapeli baada ya Rukwa na Morogoro kuwa ni Mbeya (1,112), Dar es Salaam (959) na Arusha (351) ambayo yalifanyika kwa wastani wa asilimia moja hadi 10.

Kuhusu sababu za mikoa hiyo kuongoza, alisema chanzo chake kilitokana na wahusika kutekeleza wakiwa katika maeneo hayo.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, akimbeba mtoto wakati wa harambee ya kuchangisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha watoto yatima cha "The Joy of God Ophanage Centre" kilichoko jijini Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenye selimundu wataka watu wapime kabla kuingia uhusiano

**Na Romana Mallya**

WATU wanaoishi na ugonjwa wa selimundu (sikoseli) wamesema wanatamani kuvunja mduara wa ugonjwa huo kwa watu kupima afya kabla ya kuanzisha uhusiano ndio mzizi wa tatizo.

Athari mojawapo kwa watoto wanaozaliwa na matatizo hayo ni kupata kiharusi. Athari nyingine kwao ni pamoja na kupata matatizo ya afya ya akili kunakochangiwa na maumivu makali ya mara kwa mara wayapatayo.

Shujaa wa selimundu, Arafa Said, alitoa rai hiyo juzi wakati wa kikao cha Mpango Mkakati cha Magonjwa Yasiambukiza kilichoandaliwa na Chama cha Magonjwa Yasiyoambukiza (TANCDA).

"Mimi ni shujaa wa magonjwa yasiyoambukiza, nina selimundu, ugonjwa huu ni wa kurithi kutoka kwa wazazi wote wawili, yaani baba na mama.

"Changamoto kwa tunaoishi na selimundu, huja na madhara mengine mengi zaidi kwa sababu ni ugonjwa ulio kwenye damu, unapita kuanzia kichwani mpaka miguuni, kila kiungo kinachopitisha damu kinaweza kuathirika kutokana na selimundu.

"Mojawapo ya athari ya selimundu ni watoto kupata kiharusi. Pia mtu anaweza kupata matatizo ya afya ya akili kwa sababu ya maumivu ya mara kwa mara, hivyo akili haiwi sawa," alisema.

Kutokana na athari hizo, Arafa mwenye mtoto mmoja sasa, alisema anatamani kwa pamoja wavunje mduara wa selimundu kwa watu kupima na kutambua afya zao mapema.

Alisema kila mmoja kabla ya kuanzisha familia ni lazima kumjua mwenza wake amebeba vinasaba gani.

"Lakini, kuna kaka na dada zetu ambao tayari wameshaanzisha familia hatujachelewa, pale tunapopata mtoto tumpime mapema ili kumsaidia kupata matibabu mapema. Tunaomba jamii isiwanyanyapae wagonjwa wa selimundu," alisema.

Kwa mujibu wa tovuti ya Wizara ya Afya, Februari Mosi, Waziri wa Afya (wakati huo) Ummy Mwalimu, alipotembelea watoto waliopandikizwa uroto Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma, alisema mpaka kufikia Juni, mwaka huu, serikali ilikuwa imetoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya kutibu watoto 20 wenye ugonjwa wa selimundu.

Novemba 8 mwaka jana, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, wakati akijibu swali bungeni kwa niaba ya Waziri wa Afya, alisema kuwa takribani watu 200,000 nchini wana ugonjwa wa selimundu na watoto 11,000 huzaliwa wakiwa na ugonjwa huo unaohusisha kurithi vinasaba toka kwa wazazi kila mwaka.

Kwa mujibu wa takwimu za Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya (MTUHA), jumla ya wagonjwa 86,990 wa selimundu walihudumiwa kwa mwaka 2022.

Ugonjwa wa selimundu unatambuliwa kwa kipimo cha rahisi cha damu ambacho huonesha kama mtu ana ugonjwa huo au urithi wa selimundu.

Ni ugonjwa wa kurithi unaotokana na kuwapo seli za damu zenye umbo tofauti na la kawaida. Mtu mwenye tatizo hili huwa na changamoto ya kupungukiwa damu mara kwa mara, maumivu ya kichwa, viungo na misuli.

Awali, katika kikao hicho cha mpango mkakati cha TANCDA juzi, Mtaalamu wa Afya na Mazoezi wa chama hicho, Dk. Waziri Ndonde, aliikumbusha jamii kuacha tabia bwete na kushughulisha mwili kwa kufanya mazoezi yaliyosahihi ili kujilinda na magonjwa yasiyoambukiza.

Dk. Ndonde alisema mwongozo wa ufanyaji mazoezi wa Wizara ya Afya unataka mtu afanye mazoezi angalau dakika 150 kwa wiki kwa uzito wa kati kama vile kutembea na shughuli nyingine.

Vilevile, alisema unataka mtu afanye mazoezi walau dakika 75 kwa wiki kwa mwenye uzito wa juu ikiwa ni pamoja na kukimbia, kucheza muziki kwa haraka kwa kuhusisha mazoezi ya misuli.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zichukuliwe kudhibiti ajali mwishoni mwa mwaka

**ZIKIWA** zimebaki siku 69 kumaliza mwaka wa 2024, tayari ajali za barabarani zimeibuka na kugharimu maisha ya watu. Majira kama haya, ajali kama hizo zimekuwa zikipamba moto hivyo kusababisha watu kupoteza maisha na wengine kujeruhiwa na kupata ulemavu wa kudumu.

Ndani ya wiki moja tangu Jumamosi iliyopita, kumetokea ajali tatu za barabarani ambazo zimesababisha watu 27 kufariki dunia na wengine 78 kujeruhiwa. Ajali hizo zimetokea katika mikoa ya Kilimanjaro na Mwanza.

Katika ajali iliyotokea Oktoba 19, mwaka huu, katika eneo la Kikavu, Hai mkoani Kilimanjaro, iliyohusisha magari matatu yakiwamo Toyota Coaster na malori mawili, kwa mfano, watu 14 walifariki dunia ama papo hapo au hospitalini wakati wakipatiwa matibabu na wengine 12 kujeruhiwa.

Wakati taifa likitafakari tukio hilo, juzi ziliibuka habari zingine za vifo vya watu 13 na wengine 59 kujeruhiwa katika ajali mbili tofauti. Ajali ya kwanza ni ile iliyohusisha mabasi ya Nyehunge na Asante Rabi kugongana katika eneo la Ukiliguru, Misunwi mkoani Mwanza na kusababisha vifo vya watu wanane na kujeruhi wengine 39.

Ajali ya pili ilitokea usiku wa kuamkia juzi katika eneo la Kirinjiko, wilayani Same, Kilimanjaro ambayo ilisababisha vifo vya waimbaji watano wa Kwaya ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP) Usharika wa Wazo, Dar es Salaam. Katika ajali hiyo pia waimbaji wengine 20 waliokuwamo katika Toyota Coaster walijeruhiwa.

Kwa takwimu hizo, ajali hizo zimesababisha kutoweka kwa nguvu kazi ya taifa na watu waliokuwa wakihitajika sana katika familia na jamii kwa ujumla, hivyo ni pigo kubwa. Sababu zinazoelezwa kuwa chanzo cha ajali hizo ni zile zile zikiwamo madereva kutokuwa makini kwa kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari na kusinzia kwa uchovu.

Wahenga wanasema dalili ya mvua ni mawingu. Kwa msemo huo ni kwamba hizo ni kama salamu za mwisho wa mwaka kwamba mambo yameshaanza. Hali hiyo pia inatoa ujumbe kwa vyombo vilivyopewa jukumu la kusimamia usalama barabarani kwamba vikae chonjo mambo yameshaanza.

Kama ilivyo ada, ifikapo mwishoni mwa mwaka, ajali kama hizo zimekuwa zikiripotiwa mara kwa mara ambazo zimekuwa zikisababisha watu kupoteza maisha na wengine kujeruhiwa, hivyo kubaki na ulemavu wa kudumu.

Kuwapo kwa ajali hizo na sababu zikielezwa kuwa ni mwendokasi, madereva kutokuchukua tahadhari wakati wa kuyapita magari mengine na uzembe au usingizi wa madereva kusinzia kwa sababu ya uchovu.

Ni wakati mwafaka sasa kwa vyombo vya usimamizi wa usafiri na usafirishaji kama vile Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) kuchukua hatua zinazostahili ili kudhibiti na kupunguza matukio hayo.

Bila shaka, kuwapo kwa matukio hayo yanayojirudia mara kwa mara huku nguvu kazi ya taifa ikiathirika, kuna tatizo mahali ambalo linapaswa kupatiwa ufumbuzi. Kama ni sheria kutokuwa kali, basi ni wakati mwafaka kuifanyia mabadiliko ikiwamo faini na adhabu zinazotolewa kuongezwa makali zaidi.

Aidha, ni vyema vitengo vya ukaguzi wa mabasi ya abiria vikaimarishwa ili kusiwapo mwanya wa kuruhusu magari mabovu au yenye kasoro kuingia barabarani, hivyo kusababisha ajali na kugharimu maisha ya watu.

Ni matumaini kwamba iwapo kutakuwa na usimamizi wa kutosha ikiwamo kuchukua hatua zinazostahili, Tanzania bila ajali inawezekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Jamii inahitaji elimu, hatua zaidi kuepuka janga la moto

Na Mwandishi Wetu

**HADI** sasa elimu ya kukabiliana na majanga inatakiwa kutiliwa mkazo katika jamii, ili kunusuru vifo vya watu na uharibifu wa mali zao.

Kila mara imekuwa ikiripotiwa matukio ya watu kufa kwa kusombwa na maji, ajali, vyombo vya moto, nyumba kuungua na wengine kuangukiwa na kuta.

Wananchi wamekuwa wakiitupia lawama serikali na mahsusi Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, ikidaiwa kushindwa kunusuru wakati wa majanga hayo yanatokea.

Ila kuna ushahidi wa wengi, kuwapo ujenzi holela wa makazi, ambao nao unachangia maafa hasa ya moto.

Kunashuhudiwa mahali hapo hakuna barabara za kupitisha magari ya jeshi hilo, kupeleka maji ya kuzimia moto na wataalamu husika kutumika inavyopaswa kwa ujuzi na nyenzo nyingine walizo nazo.

Kinyume chake, kila kunapozuka moto, wakazi wake wamekuwa wakitumia mchanga na maji kuzima moto, bila ya mafanikio. Hiyo ni kutokana na kukosa elimu sahihi ya kukabili janga hilo.

Vilevile, wakati wa mvua, mafuriko yamekuwa yakisababisha madhara kwa jamii tajwa jirani.

Ni aina ya madhara yanayowagusa watu, hususani watoto wanasombwa na mafuriko, wanakutwa wameshakufa.

Vilevile majanga ya vifo kwa watu kutumbukia visimani, madimbwi na mashimo ya vyoo, tahadhari ingeweza kuchukuliwa endapo jamii ingepata elimu sahihi.

Ni kawaida kukuta choo kina nyufa, hali kadhalika madimbwi, mito kujaa, lakini watu wanashindwa kuchukua tahadhari, wanaendelea kutumia kukumbwa na mkasa wa maafa.

Kimsingi, hiyo ni mifano michache, ila kuna mingi inapatikana kwenye makazi ya watu.

Inashauriwa kabla ya kuanza ujenzi wa makazi kupeleka ramani za nyumba katika mamlaka ya kitaalamu kisheria ya ujenzi, kwa ajili ya ushauri wa namna ya kukabiliana na majanga hayo, ili wapatiwe msaada sahihi.

Ushauri huo ni pamoja na ujenzi wa nyumba kwa mpangilio, unaotoa fursa kwa watu kupita na magari ya zimamoto kwenda kuokoa, panapokuwapo hitaji.

Ukweli ulioko ni kwamba, nyumba nyingi zimekuwa zikitetekea na watu wengi kufia ndani, kwa kukosa msaada wa kikosi hicho cha kuzima moto na uokoaji, kutokana na magari husika kukosa barabara ya kupita hadi kwenye tukio stahiki.

Kinachofanyika mara nyingi, ni kwa baadhi ya wajuzi na wahusika wa tukio kuamuru umeme uzimwe, ili kudhibiti moto kusambaa kwenye majengo mengineyo, hata yakaleta madhara zaidi.

Hiyo yote inatokana na uhalisia nyumba nyingi ziko katika maeneo yasiyopimwa na kimsingi, baadhi zipo katika maeneo yaliyoachwa wazi kwa huduma maalum, baada ya viwanja kupimwa, mathalan mahsusi kwa kupitisha maji wakati wa mvua.

Iko busara ya kukubaliana na ukweli kwamba, pamoja na serikali kuwekeza fedha nyingi kukabiliana na majanga ya namna hiyo, pia jamii inapaswa kuweka mkazo kwenye utoaji elimu ya umma, kuzingatia kanuni na taratibu za miundombinu wakati wa ujenzi wa nyumba zao.

Hata kwa maeneo yasiyopimwa, vilevile kuna mkondo wa kisheria unaomtaka mjenzi kupata kibali cha serikali ya mtaa husika. Hapo kunakuwapo maelekezo ya kufanikisha kwa usahihi na kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazosimamia ardhi nchini.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amesikika akizungumzia kuwapo mpango unaotengeneza utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi, kuhusu kinga na tahadhari ya moto.

Kinachodhamiriwa hapo ni kuwawezesha kuwa sehemu ya jitihada za kudhibiti majanga hayo nchini.

Masauni anaitaja kuwa elimu inayowasaidia wananchi kuzuia kutokea moto unaowaachia watu vifo, ulemavu na uharibifu wa mali kwa watu.

Anasema hata yanapotokea majanga ya moto na ajali, wananchi wenye elimu sahihi wanaweza kutoa ushirikiano chanya kwa askari Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Mpango wa jeshi hilo unatajwa ni kutoa elimu sahihi kwa wananchi, hali inayowasaidia kupunguza moto na majanga mengine ya namna hiyo kwenye makazi, ajali za barabarani na majini.

Elimu hiyo pia inatajwa kusaidia kunusuru mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya biashara na usalama wa mazingira, pia mazao, hata magari yanayonusuriwa kuteketea kwa moto.

# Mwinyi aahidi fedha zaidi sekta ya elimu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali itaendelea kuongeza fedha kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuwa ni sekta ya kipaumbele kwa maendeleo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Mawasiliano, Ikulu Zanzibar, Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipofungua shule mpya ya sekondari ya ghorofa tatu, Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja, ikiwa ni mwendelezo wa wiki ya kupongeza juhudi za serikali ya awamu ya nane kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wake.

Dk. Mwinyi alisema uzinduzi wa shule hiyo ni kuimarisha mifumo na miundombinu ya elimu ili kufanikisha mageuzi makubwa yanayoendana na teknolojia ya sasa duniani.

"Hii ni dunia ya teknolojia, hivyo tunaweka kipaumbele katika kuimarisha teknolojia ili vijana waende sambamba na mabadiliko ya dunia na kuongeza ufaulu wao," alisema.

Alisema fungu kubwa la bajeti hiyo litaelekezwa zaidi kwenye kuimarisha mifumo ya elimu, ujenzi wa miundombinu ya shule za kisasa ikiwamo maabara, vyumba vya kompyuta, maktaba na kumbi za mikutano ambazo hutumika kufanyia mitihani.

Dk. Mwinyi alisisitiza kuwa hadi sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imetengewa Sh. bilioni 830 ambazo zinatarajiwa kuongezeka hadi kufikia Sh. trilioni moja kutoka bajeti ya miaka mitatu nyuma ya Sh. bilioni 83.

Pia alisema serikali imejenga madarasa 2,738 kwa kuvuka lengo la Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 - 2025 ambayo ilielekeza kujengwa madarasa 1,500. Alisema hatua hiyo inakusudia kutekeleza azma ya serikali ya kuhakikisha wanafunzi 45 wanasoma kwa mkondo mmoja katika darasa moja huku serikali ikiweka mkazo zaidi kwenye masomo ya hisabati na sayansi.

Kuhusu maslahi ya walimu, Dk. Mwinyi alisema serikali itaendelea kuongeza hasa kwa wanafanyakazi wenye mazingira magumu.

Aidha, kuhusu ajira mpya, alisema serikali imeajiri walimu 3,600 na inalenga kuongeza ajira za walimu zaidi hasa kwa kada za sayansi na hesabati.

Rais Mwinyi alieleza kufarajika na mafanikio makubwa katika sekta ya elimu ambayo yamechangia kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kufikia asilimia 96.6 kwa kidato cha sita na asilimia 88 kwa kidato cha nne kutoka asilimia 55 kabla ya miaka minne ya uongozi wake.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema ujenzi wa shule za ghorofa Kaskazini, Unguja umewaletea faraja wazazi na wanafunzi wa mkoa huo kwa tatizo la umbali wa kufuata elimu katika skuli za mjini.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, alimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa kuiletea mageuzi makubwa sekta ya elimu kwa kuweka fedha nyingi za kutekelezwa miradi mbalimbali ya elimu.

Alisema jitihada hizo ikiwamo kuwekeza vifaa na miundombuni ya kisasa ya kufundishia, zitasaidia kwenye mchango wa maendeleo ya taifa kwa kutoa wataalamu wa kutosha watakaokuwa tayari kushindana katika soko la ajira duniani.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdalla Said, alisema ujenzi wa shule hiyo ulianza Mei, 2023 na kukamilika Oktoba, mwaka huu na umegharimu Sh. bilioni 6.1, alisema shule hiyo ina madarasa 42, matundu ya vyoo 52, chumba cha kompyuta, maabara, maktaba na shule hiyo itachukua wanafunzi 1,890 kwa wakati mmoja.



Meneja Mwandamizi Biashara wa Benki ya Azania, Jackson Lohay akizungumza na wafanyabiashara ambao in wateja wa benki hiyo walipowasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere wakitokea China ambako walipelekwa kuhudhuria Maonesho ya Canton Fair.Takriban wafanyabiashara 40 kutoka maeneo mbalimbali nchini walidhaminiwa na Benki ya Azania kushiriki maonesho hayo kwa muda wa wiki mbili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dar kupambwa kwa taa, kamera za usalama

**Na Joseph Mwendapole**

MKOA wa Dar es Salaam umeanza kuweka taa na kamera za usalama katika maeneo mengi ya jiji hilo kama mkakati wa kurahisisha usalama na kuwawezesha wafanyabiashara kufanya shughuli zao kwa saa 24.

Hatua hiyo ilitangazwa jijini Dar es Salaam na Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila, wakati wa ziara yake usiku wa kuamkia jana katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

Chalamila alitembelea na kukagua ujenzi wa barabara ya mwendokasi (BRT III) inayoanzia maeneo ya Posta hadi Gongo la Mboto, shule za Azania na Jangwani na Soko la Kariakoo.

Alisema watahakikisha maeneo mengi yanakuwa na taa na kamera za usalama ili kila atakayefanya uhalifu, afahamike na kuchukuliwa hatua za kisheria kama fundisho kwa wengine.

"Hivi karibuni nilitembelea moja ya nchi zilizoendelea, mwanamke mmoja aliibiwa pochi yake, ndani ya saa saba aliitwa akaoneshwa aliyemwibia na pochi yake ikapatikana. Sasa jiulize kwa sasa hapa Kariakoo mtu akiiba pochi itapatikana kirahisi namna hiyo?

"Ndiyo maana tunataka kupendezesha mji wa Dar es Salaam kwa kuupamba na taa na kamera kiasi kwamba watu wanaotoka mikoani wakifika tu wajue kwamba hapa ni Dar es Salaam! Kuna kampuni imejitolea, inaweza kufunga taa za mfano na mkiridhika nazo wapeni kazi hiyo," alisema.

> **Alisema kuwa baada ya kuhakikiwa, majina hayo yataingizwa katika mfumo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili soko hilo lifunguliwe na kuanza kufanya..**

Chalamila alisema Manispaa za Jiji hilo zimeshaanza kufunga taa kwenye baadhi ya maeneo na aliagiza kazi hiyo iwe endelevu na ikamilike ndani ya muda mfupi ili kuwawezesha wafanyabiashara kufanya kazi wakiwa na uhakika wa usalama wa biashara zao.

Akizungumzia Soko la Kariakoo, Chalamila alisema linakarabatiwa kwa Sh. bilioni 28 na mradi huo umefikia zaidi ya asilimia 92 na majina ya wafanyabiashara watakaokuwa kwenye soko hilo yanahakikiwa kwa awamu ya tatu.

Alisema kuwa baada ya kuhakikiwa, majina hayo yataingizwa katika mfumo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili soko hilo lifunguliwe na kuanza kufanya kazi haraka.

Mkuu wa Mkoa alipongeza Shirika la Nyumba (NHC) kwa uamuzi wake wa kuyavunja majengo ya zamani na kuingia ubia na wafanyabiashara binafsi kujenga majengo marefu ya kwa ajili ya makazi na biashara.

Alisema ujenzi wa majengo hayo marefu utapendezesha Kariakoo kuwa mji wa kisasa na unaovutia kwa kuwa majengo yaliyoko yamechakaa na hayachukui wapangaji wengi kama itakavyokuwa kwa majengo mapya yatakapokamilika.

"Majengo mengi yatakuwa ya zaidi ya ghorofa 10 na kutakuwa na maduka na makazi ya kupanga ambayo yatawarahishia wafanyabiashara kutoka mikoa mbalimbali na mataifa ya kigeni kupata makazi ya muda wanapokuja kuchukua mizigo.

"Kwa sasa mabasi yanafanya kazi saa 24 kutoka mikoa mbalimbali. Swali limebaki; je, abiria watakaposhuka wataelekea wapi, hasa wale ambao wanakuja kuchukua mizigo Kariakoo?

"Ndiyo maana Rais akaagiza kwa kuwa ruti za mabasi ni saa 24, safari za ndege na usafiri wa SGR (reli ya kisasa) upo ni vyema Kariakoo ikawa wazi kwa saa 24," alisema.

Meya wa Jiji la Ilala, Omar Kumbilamoto, alisema mapendekezo yatakayoletwa kwenye Baraza la Madiwani kuhusu mipango ya kuboresha jiji kwa kuweka kamera na taa za usalama, yatapitishwa kwa utekelezaji wa haraka.

"Ninampongeza Mkurugenzi wa Jiji la Ilala kwa maono yake ya kuhakikisha jiji hili linakuwa na taa na kamera za kutosha.

"Tumepakana na wilaya za mkoa wa Pwani na wilaya mbalimbali, hivyo nikuhakikishie (Mkuu wa Mkoa Chalamila) tutaweka taa ili watu wote wakifika Dar tu, waone mwanga wa kutosha, hatutaki kuona maeneo yetu yako gizani," alisema.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa serikali yake kukubali kutoa Sh. bilioni 28 za ukarabati wa Soko la Kariakoo lilipoungua na Sh. milioni 100 zilizotumika kuwajengea wafanyabiashara waliokuwa hapo maeneo ya muda.

## KABWELA   Na Fadhili Mohammed





Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing Investment, Fred Msemwa, akionyesha tuzo ya nyumba za gharama nafuu zaidi Afrika iliyotolewa na Taasisi ya Mikopo ya Nyumba Afrika (AUHF). Tuzo hiyo imetolewa katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa AUHF uliofanyika Zanzibar wiki iliyopita. Kushoto ni Mkurugenzi wa Uendeshaji, Sephania Solomon na kulia ni Raphael Mwabuponde, Mkuu wa Kitengo cha Masoko, na Mwanasheria Mkuu wa WHI, Joel Maeda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makalla: CCM itaheshimu matokeo yoyote

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU wa NEC Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, amesema watakuwa chama kiongozi cha kuheshimu matokeo yoyote yatakayotokana na uchaguzi ujao ambao wanaamini utakuwa huru na wa haki.

Amesema wanasubiri muda ufike wakafanye kampeni za kistaarabu na baada ya uchaguzi, aliyeshinda uchaguzi kwa haki, atatangazwa mshindi na aliyeshindwa atatakiwa kupokea matokeo hayo.

Makalla amesema CCM haihitaji 'mbereko' na kwamba kutokana na kazi waliyofanya, wanaamini wananchi watawaelewa.

Makalla alieleza hayo juzi mkoani Dar es Salaam wakati akipokea taarifa ya hali ya uandikishaji wananchi katika Daftari la Wakazi, akiwapongeza viongozi wa kichama katika mkoa huo kwa kufanikiwa kuandikisha watu milioni 3,480,630 sawa na asilimia 96.7 ya lengo la kuandikisha wapigakura milioni 3,599,247.

"Nitoe wito kwa upinzani, zoezi hili la uandikishaji liwe funzo kwao kwamba umma hauandaliwi kwa nguvu, kutengeneza matukio na propaganda za muda mfupi, bali unaandaliwa kwa kukubali yale mambo yanayohusu jamii yenyewe, hiyo ndio falsafa ya maandalizi ya umma.

"Wenzetu ambao muda wote wamekuwa wakosoaji, jambo hili Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wajifunze kwamba hawakujipanga, hawakuwa na maandalizi ya uchaguzi, hawakuwa wamoja, tumekisema kina mgawanyiko mkubwa," alidai Makalla.

"Kwa sababu Watanzania ni waelewa, wameshindwa kuichafua Tanzania kwa kuharibu amani. Siri kubwa watu ni waelewa, wengine vinara wa kuchochea familia zao ziko mbali ya nchi hii ikiwamo Canada. "Sisi Watanzania tubaki wamoja, tunapoelekea katika uchaguzi tukosoane kwa hoja kwa ustaarabu wa R4, tukishindwa mtaa fulani, tutajipa funzo kwanini tumeshindwa," alisema Makalla.

Alieleza kuwa haina maana watu kuanza kusumbua wengine kwenye vituo, kutaka kuwapiga na kuwafanyia fujo, akisema kwamba huo ni "ushamba wa siasa na si ustaarabu katika R4".

Makalla alisisitiza kwamba yeyote atakayeanguka katika uchaguzi ujao, lazima aangalie amekosea wapi na si kwenda kuleta vurugu.

Alisisitiza kuzingatia amani, kanuni na sheria zilizowekwa kuelekea kwenye uchaguzi, akiahidi wananchi kwamba baada ya kukamilisha zoezi la uandikishaji, CCM itateua wagombea safi wanaokubalika.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)
ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 5(1) ya Kanuni za Mafuta (Compressed Natural Gas) (Supply and Marketing Services Rules, GN No. 220 of 2019).**

**TAARIFA** TAARIFA inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji **(EWURA)** imepokea ombi la kibali cha ujenzi wa kituo cha kujaza gesi asilia iliyoshindiliwa kwenye magari kutoka **PUMA ENERGY TANZANIA LIMITED** kitakacho jengwa Kiwanja namba 1 Kitalu D, eneo la huduma za biashara Mbezi Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam.

Hivyo, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;
Namba ya Bure 0800110030;

Barua pepe: **info@ewura.go.tz** Tovuti: **http://www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz

# Maofisa JWTZ wasimika Mwenge Mlima Kilimanjaro

**Na Mary Mosha,** MOSHI

LUTENI Kanali, Khalid Khamis Khalid na kikosi cha maofisa na askari 21 wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wamemaliza kibarua cha kupandisha Mwenge wa Uhuru na Bendera ya Taifa katika Kilele cha Mlima Kilimanjaro Uhuru.

Jana, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, aliwapokea mashujaa hao waliotumia siku sita kutekeleza amri ya Rais Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa Oktoba 14 mwaka huu, mkoani Mwanza, wakati wa kilele cha mbio za mwenge huo wa uhuru kitaifa.

Mara ya kwanza (Desemba 9, 1961), Mwenge huo ulipandishwa katika kilele cha Uhuru, chenye urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa Bahari na Luteni Kanali (wakati huo), Alexander Nyirenda.

Wakati huo katika Mji Mkuu wa taifa jipya la Tanganyika, Dar es Salaam, bendera ya taifa, ilikuwa ikipandishwa Uwanja wa Taifa, baada ya kushushwa bendera ya Uingereza.

Mara ya pili, ilikuwa Desemba 5, 2011, Tanganyika ilipofikisha miaka 50 ya Uhuru.

Waziri Tax alisema kuwa: "Kama mlivyopewa jukumu hili zito na Rais Samia Suluhu Hassan la kupandisha Mwenge na bendera ya taifa katika kilele cha Mlima Kilimanjaro, ninayo heshima kubwa kuwapokea mkiwa salama na mmekamilisha kazi mliyopewa kwa uaminifu, tena kwa umahiri na nguvu ya ajabu.

...Mmeendelea kuliheshimisha jeshi letu na kamwe halitarudi nyuma katika kulitumikia taifa. Natambua haikuwa kazi rahisi, lakini mmekabiliana nayo kwa uzalendo mkubwa."

Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi nchini, Jenerali Jacob Mkunda, alipokutana na kikosi hicho, alisema kama alivyopewa jukumu la kupandisha Mwenge pamoja na bendera Mlima Kilimanjaro, sasa yupo tayari kupeleka taarifa kwa Rais Samia, kwa mujibu wa itifaki.

"Tutaendelea kutekeleza majukumu kizalendo kwa lengo la kuleta matokeo chanya kwa taifa letu," alisema Jenerali Mkunda.

Oktoba 15, mwaka huu, Mwenge huo ulianza safari hiyo kupitia lango la Marangu la Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA).

# Vifo vya njiti 'pasua kichwa' duniani

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MADAKTARI na waguzi gwiji 220 kutoka nchi 28 duniani wanakutana jijini hapa kuweka mikakati ya kukabiliana na vifo vya watoto wanaozaliwa njiti kwa kutoa huduma bora.

Jana Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Watoto Wachanga na Vijana wa Wizara ya Afya, Dk. Felix Bundala, alisema magwiji hao wanakutana kujengeana uwezo kutokana na kila nchi kukabiliwa na vifo vya watoto hao.

"Kongamano hili la nne la mafunzo kwa wataalamu hawa ni muhimu sana kusaidia kupunguza vifo vya watoto wachanga," alisema Dk. Bundala.

Alisema kongamano hilo linafanyika baada ya kushuka kwa vifo vitokanavyo na uzazi kwa asilimia 80 kutoka 556 mwaka 2016 hadi vifo 101 mwaka 2021.

"Kimsingi, mafunzo tunayofanya hapa Arusha, lengo lake pia ni kuendeleza mkakati wa kupunguza vifo vya mama na mtoto, hasa wenye umri chini ya miaka mitano, wakiwamo wanaozaliwa kabla ya wakati (njiti)," alisema na kuongeza kuwa: "Watoto chini ya umri wa miaka mitano, vifo vyao vimepungua kwa asilimia 40 kutoka 97 hadi 43 kwa vizazi 1,000 katika kipindi hicho cha mwaka 2016 hadi 2021."

**Kwa Tanzania, Wizara ya Afya, imeeleza nia yake kutaka kuongezwa kasi ya ujenzi wa wodi maalum za watoto wachanga nchini, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, alilolitoa Oktoba**

Kwa Tanzania, Wizara ya Afya, imeeleza nia yake kutaka kuongezwa kasi ya ujenzi wa wodi maalum za watoto wachanga nchini, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, alilolitoa Oktoba mwaka jana.

`Hadi kufikia Juni mwaka huu, hospitali ambazo zimeanzisha wodi hizo nchini zimeongezeka kutoka 14 zilizokuwapo mwaka 2018 hadi kufikia 250.

Mjumbe wa Taasisi ya Afya ya Mtoto Afrika (ICHA), Remla Shirima, alisema kongamano hilo linalenga zaidi kuwajengea uwezo wataalamu hao wakiwamo 23 kutoka Bara la Afrika kuhudumia watoto njiti.

Ofisa Muuguzi Wodi ya Watoto Wachanga ya Hospitali ya Maternity Africa, Ndini Itoine, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kuongeza uelewa wa kuhudumia watoto njiti.



Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Tanga, Dk. Fani Mussa (kulia), akiwaongoza madaktari bingwa wa Samia Suluhu kukagua majengo ya hospitali hiyo jana. Madaktari hao wamefika katika wilaya hiyo kwa ajili ya kutoa huduma za kibingwa kwa wananchi kupitia kambi ya siku sita kuanzia juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kortini kwa madai ya kumuua mwanawe

**Na Allan Isack,** KITETO

MKAZI wa Kijiji cha Orkitikiti wilayani hapa Mkoa wa Manyara, Jeremiah Kwang (32), amefikishwa mahakamani kujibu shtaka la mauaji ya mtoto wake mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu.

Mshtakiwa huyo alifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kiteto jana mbele ya Hakimu Mkazi, Mossy Soro.

Akisoma hati ya mashtaka, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Wilfred Mollel, alidai kuwa Oktoba 5, mwaka huu, mshtakiwa huyo alimuua mtoto huyo, John Kwang nyumbani kwake katika Kijiji cha Orkitikiti.

Aliendelea kudai kuwa mshtakiwa huyo, alimuua mtoto wake kwa kumpiga chini mara kadhaa na kusababishia majeraha mwilini

Alidai baada ya mshtakiwa huyo kumsababishia majeraha mtoto huyo, alipelekwa zahanati na kufariki wakati madaktari wakimpatia matibabu.

Mshtakiwa huyo hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo, haina uwezo wa kusikiliza kesi hiyo ya mauaji hadi atapofikishwa Mahakama Kuu.

Hakimu Soro, aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 29 mwaka huu, itakapotajwa mahakamani hapo.

# Shehena nyingine yatua bandarini Tanga

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MELI ya Seafront yenye shehena ya magari makubwa ya mizigo zaidi ya 300 na bidhaa nyingine mchanganyiko, imetia nanga kwa mara ya pili katika Bandari ya Tanga jijini hapa.

Ofisa Habari wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchini (TPA), aliyemwakilisha Mkurugenzi Mkuu katika mapokezi, kabla ya upakuaji wa mizigo hiyo jana, Enock Bwigane, alisema Kampuni ya Seafront Shipping Ltd ni tegemeo katika utumiaji wa bandari hiyo baada ya kufanyiwa ukarabati mkubwa.

Shehena ya bidhaa na magari mengi yanayoingizwa nchini na meli hiyo, zinapelekwa nje ya nchi kupitia bandari hiyo iliyoko mkoani Tanga.

"Uwekezaji uliofanywa na serikali wa Sh. bilioni 429.1 kuboresha Bandari ya Tanga, umesababisha sasa meli kubwa nyingi na shehena tofauti kushushwa katika bandari hii.

Huyu ni mteja mmoja wapo anayeleta mizigo kutoka nchini China," alisema.

Kutokana na maboresho ya bandari hiyo, mapato yameongezeka na kuanzia Julai mosi hadi Septemba 30 mwaka huu hadi kufikia Sh. bilioni 18.6, katika hizo bilioni nane zimetokana na Kampuni Sea Front.

Bwigane, alisema ufanisi, mapato na shehena vinaongezeka kila mwaka. Miaka miwili iliyopita, shehena tani 800,000 zilihudumiwa na sasa zimefikia milioni 1.1, huku wakitegemea nyingine milioni 1.4 mwaka huu.

"Katika robo tatu ya kwanza mwaka huu, tumeshahudumia tani 300.3. Tunapiga hatua kubwa katika kushusha shehena nyingi Tanga, pia katika ushoroba wa kaskazini," alisema.

Awali, Meneja wa Bandari hiyo, Masoud Mrisha, alisema kutokana na uboreshwaji huo, ajira nyingi kwa vijana zimeongezeka kupitia ongezeko la kampuni, ambazo zimesajiliwa kufanya kazi.

Alisema kabla ya maboresho hayo kulikuwa na kampuni 32 zilizosajiliwa, kwa sasa zimesajiliwa nyingine 132.





# Watakiwa kunusuru watoto 'uteja'

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAZAZI na walezi wametakiwa kufuatilia mienendo ya watoto ili kuwanusuru kutumia dawa za kulevya na kutimiza ndoto zao katika maisha yao ya baadaye.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Kupambana na Kupinga Matumizi ya Dawa za Kulevya la Simama Tena Foundation (STF), Grace Nzagamba, wakati akitoa mrejesho wa utafiti kuhusu matumizi ya dawa hizo miongoni mwa vijana wakati wa uzinduzi wa shirika hilo katika Mtaa wa Shinu lenye uwezo wa kuhudumia waraibu 20.

Nzagamba, alisema katika utafiti walioufanya kwa walimu, wanafunzi, wazazi, waraibu, waandishi wa habari na viongozi wa dini, walibaini vijana wengi hususani wanafunzi wanaathirika kwa kiwango kikubwa na dawa hizo hususani bangi.

Alisema ni muhimu wa wazazi kujihusisha na malezi ya watoto wao kwa kuzungumza nao kuhusu madhara ya dawa hizo na unywaji pombe kwa kuharibu nguvu kazi ya taifa.

Alisema wazazi wengi wanashindwa kugundua tabia za watoto wao hadi wanapopewa taarifa na walimu, hali inayofanya suala la malezi kuwa changamoto kubwa baina yao.

"Watoto wengi hugunduliwa na walimu huku wazazi wakiwa hawaelewi lolote kuhusu tabia za vijana wao kujiingiza kwenye utumiaji wa bangi na gundi," alisema Nzagamba.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Kahama, Dk. Baraka Mfumi, alisema serikali inaendelea kutoa elimu kwa jamii kuacha kutumia dawa hizo na kuwapatia matibabu walioathirika.

Awali akishuhudia madhira aliyokutana nayo katika uraibu, Meneja wa STF, Ally Baden, alisema dawa hizo zilisababisha kuwa mwizi mitaani.

Baden, alisema aliondokana na hali hiyo aliyoishi nayo muda mrefu baada ya kupewa tiba ya uhakika kupitia nyumba za kutibu waathirika na dawa hizo jijini Dar es Saalam.

Alisema amekuwa mfano wa kuigwa kwenye jamii kwa kukutana na vijana na kuwaeleza madhara yake na kuwashawishi kuacha.

Mmoja wa waraibu wilayani hapa, Ally Farhan, alishauri watumiaji wa dawa hizo wasinyanyapaliwe badala yake wasaidiwe, kuaminiwa na kupendwa ili kujiweka karibu na jamii na kuweza kuondokana na hali hiyo.

# Chanzo cha maji KASHWASA shakani

**Na Marco Maduhu,** MISUNGWI

MADAKIO ya chanzo cha maji cha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama na Shinyanga (KASHWASA) yamevamiwa na shughuli za kibinadamu na kusababisha kushuka uzalishaji maji kwa ajili ya matumizi ya wakazi wa mikoa minne nchini.

Chanzo hicho kinatoa maji hayo kutoka Ziwa Victoria na kusambaza mikoa hiyo ya Mwanza, Kahama, Shinyanga, Tabora, Singida na Geita.

Hayo yalibainishwa na Meneja Biashara wa KASHWASA, John Zengo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo wakati alipotembelea Mamlaka ya Maji Kahama (KUWASA) kilipo chanzo hicho.

Kwa mujibu wa Zengo, uvamizi huo ambao umesababisha kukumbwa na uharibifu wa mazingira unafanywa na baadhi ya wananchi wanaoishi kukizunguka kwa kuendesha shughuli za kilimo na kujenga nyumba.

"Hali hii husababisha maji ambayo tunavuna ndani ya Ziwa Victoria kuwa na tope jingi na kutumia gharama kubwa ya dawa za kutibu maji. Kwa mwezi tunatumia kati ya Sh. milioni 300 hadi 350 kwa mwezi," alisema Zengo.

> **"Hali hii husababisha maji ambayo tunavuna ndani ya Ziwa Victoria kuwa na tope jingi na kutumia gharama kubwa ya dawa za kutibu maji. Kwa mwezi tunatumia**

Alisema wakidhibiti uharibifu huo, watapunguza kwa kiasi kikubwa gharama za za kununua dawa hadi kufikia kati ya Sh. milioni 100 ha 50, kwa mwezi.

Alisema kwa kushirikiana na wadau, wamekuwa wakitoa elimu ya madhara ya uvamizi wa chanzo hicho na kuwataka wananchi kuacha uvamizi wa madakio hayo.

Zengo, alisema pamoja na jitihada hizo, tatizo hilo lipo pale pale kutokana na wananchi hao kuendelea kukaidi, hivyo wameanza kuchukua hatua kwa kubandika tangazo la onyo na tahadhari dhidi yao.

Mwenyekiti wa Bodi ya KUWASA, Sterwat Bulaya, aliipongeza serikali kwa uwekezaji mkubwa wa kutoa majisafi na salama kwa matumizi ya wakazi wa mikoa hiyo kutoka Ziwa Victoria.

Bulaya, aliitaka KASHWASA kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kuweka alama na mipaka kwenye madakio hayo ili kudhibiti wavamizi hao na mazingira kuharibiwa, lasivyo chanzo hicho kitashindwa kufanya kazi ipasavyo na kusababisha uhaba wa maji katika mikoa hiyo.




Baadhi ya mashuhuda wakiliangalia basi la Nyehunge baada ya kutokea ajali ya mabasi kugongana na kusababisha vifo vya watu wanane na majeruhi 39. **PICHA: ELIZABERTH FAUSTINE**

# Wajawazito wakacha kupimwa VVU

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

IDADI kubwa ya wajawazito wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga hawahudhurii kliniki siku za awali kwa lengo la kukwepa kupima Virusi Vya Ukimwi (VVU) na kumiminika miezi ya mwisho ya kujifungua, imefahamika.

Kauli hiyo ilitolewa hivi karibuni na Kaimu Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Mwendakulima kilichoko Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Dk. Leonora David wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Afya na Lishe.

Dk. David, alisema hali hiyo ina hatarisha maisha ya mtoto akiwa tumboni kwa kukosa kufahamu maendeleo ya afya yake kwa kipindi chote cha ujauzito hadi kujifungua.

Alisema wajawazito hao wanaanza huduma hiyo kuanzia miezi sita na kuendelea wakiwa wamebakiza muda mchache kujifungua bila kupima afya zao.

Alisema mjamzito anapobainika kuwa na maambukizi ya VVU wanampatia elimu ya kumkinga mtoto kabla na baada ya kujifungua.

Dk. David, alisema mjamzito anatakiwa kuwahi kliniki baada ya kujihisi kuwa na mimba yenye umri chini ya wiki 12 akiwa na mwenza wake ili kupima ukimwi, ugonjwa wa zinaa wa kaswende na homa ya ini yanayosababishwa na ngono zembe.

Aliwataka wajawazito kuacha tabia hiyo ili kulinda afya na vichanga vyao tumboni.

Daktari Bingwa wa Uchunguzi wa Magonjwa kwa Mionzi na Mawimbi, Dk. Fredrick Malunde, alisema udumavu na utapiamlo kwa watoto unasababishwa na ulaji wa vyakula ambavyo havikungatia mlo kamili.

Dk. Malunde, alisema mtoto asiyekuwa na afya bora anakuwa na uwezo mdogo wa kufikiri na kushindwa kufanya vema kwenye masomo yake.

Alisema utafiti umebaini mtoto wa kike asipopata lishe bora hasa madini chuma wakati wa makuzi yake, nyonga zake za uzazi zinashindwa kutanuka anapojifungua na kufanyiwa upasuaji, hivyo kusababisha ongezeko la vifo vya wajawazito na watoto.

Mkazi wa Mtaa wa Busalala Kata ya Mwendakulima, Esther Amos, alisema hakujua kama mtoto wa kike asipopata lishe bora ya madini chuma anaweza kushindwa kujifungua na kufanyiwa upasuaji na kuahidi kuwalisha watoto wake wote vyakula bora ili wawe na afya njema, wafanye maamuzi sahihi katika masomo yao.

ama
ALHAMISI OKTOBA 24, 2024
AFYA NA MAZINGIRA


Ukurasa 12

**UKOMBOZI MAZINGIRA...**

**Wapewa mbadala uchumi, wafanikiwa kunusuru mazalia ya samaki ufukweni**


Ukurasa 13

Wanasayansi wafukua undani Tsunami 2014 baharini, hadi enzi dunia changa


Ukurasa 14

**VITA ISRAEL NA PALESTINA WIKI HII...**

**Simulizi na ushuhuda uliotawaliwa na vifo, majeruhi, saikolojia mateso**

UBUNIFU WA 2007 UKING'ARA 'KIVINGINE'...

# Fahamu silaha kuu za Awamu Sita zinazoibua mapinduzi ya afya nchini

**Na Mwandishi Wetu**

HADI sasa kuna uwekezaji unaoendelea kutekeleza Sera ya Afya Mwaka 2007, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika staili yake anatumia namna kuu mbili kufanikisha anayolenga, katika mradi ulioasisiwa katika Serikali ya Awamu ya Tatu, kwa jina Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM).

Rais katika ubunifu wake, ameweka mgawanyo ambao katika sura moja unagusa miundombinu inayopatikana katika namna kuu mbili; huku rasilimali watu nayo kitaalamu anaikuza kwa mgawanyiko wa aina mbili.




Rais Samia Suluhu Hassan, alipozuru katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma mapema mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

### NGUVUKAZI AFYA

Eneo la rasilimali watu, serikali pia imewekeza katika kutanua idadi wataalamu afya na wakati huohuo, kuna uboreshaji tija kwa wakati mmoja safu yao, kukiwapo ajira mpya inayoongozwa kila mwaka kukidhi mahitaji ya nchi.

Hiyo inaendana na kasi ya uboreshaji kitaalamu uzalishaji mabingwa wa tiba kitaifa serikali ijitegemee, kupitia kinachoitwa Mpango wa Udahili wa Masomo ya Serikali, maarufu 'Samia Health Specialization Scholarship Program' unaopeleka masomoni wataalamu 300 kila mwaka, 2024 mwaka huu ikiwa na bajeti Sh. bilioni 14.

"Changamoto ya upungufu wa watumishi katika sekta ya afya inatokana na kukua idadi ya watu, ambayo inaongeza uhitaji wa wataalamu wa afya na walimu, lakini endapo Tanzania itakua kiuchumi changamoto hiyo itaondoka," anasema Rais Dk. Samia.

Hapo mkuu wa nchi ameamua kutumia tafsiri ya 'maendeleo na kujitegemea' katika afya kwa maana nchi kukidhi mahitaji yake kwa idadi, pia ujuzi unaopunguza safari ya tiba za ugenini kama vile nchini India, Tanzania.

Utashi wa kimaendeleo hapo ni nchi kuwa na idadi ya kutosha ya wataalamu na wenye uwezo wa kuhudumia mahitaji tiba yanayojitokeza nchini, hata kwa majirani; nyenzo za kufanyia kazi zikiwapo katika namna endelevu.

Pia, Dk. Samia anafafanua kuongezeka rasilimali watu katika Sekta ya Afya ni la mustakabali mpana, yakitegemea jitihada za pamoja, ikiwamo serikali, sekta binafsi, wadau na taasisi za kidini kuwekeza katika vichocheo vya uwekezaji, kuongeza ubora wa huduma za afya nchini.

Hadi sasa Tanzania ina sheria, pia sera inayohusu ubia kati ya sekta binafsi na serikali, maarufu PPP. Rais katika kuongeza idadi ya watumishi wa afya, anaahidi serikali itaendelea kutoa vibali vya ajira kila mwaka katika sekta ya afya, ili kupunguza uhaba wa watumishi hao, kutokana na maendeleo katika sekta hiyo.

Katika nafasi hiyo, Rais Dk. Samia anawasifu wabia, Taasisi ya Benjamin Mkapa, inayochukua hatua ya kuboresha rasilimali watu na mikataba yao inapoisha, wanaajiriwa na serikali.

Mfano wa namna ya pekee, Rais anachukua hatua hizo za kuajiri, ikishuhudiwa mapema mwaka huu mkoani Tanga, serikali iliajiri kundi la watumishi katika mgawanyiko wa madaktari wanane; wafamasia saba; wataalamu maabara 20; na wasaidizi afya 22.

Wengine wasio wataalamu afya moja kwa moja, ni wahudumu wa wateja (5); wasaidizi hesabu (8); wasaidizi ustawi jamii (4); na mtunza kumbukumbu mmoja.

Badaaye, Julai mwaka huu kukaonekana tangazo ligine la kukaribisha maombi ya watumishi afya nchini 9,483 kutumika mikoa: Arusha (9), Dar es Salaam (3), Geita (38), Iringa (26), Kagera (18) na Katavi (32).

Manufaa yake ndio kinachoshuhudiwa kuwapo kikosi cha wataalamu wajuzi tiba kutoka Hosptali ya Taifa wanaozunguka kitaifa kusambaza ujuzi tiba na wakati huo huo, wanatoa huduma kuhusu watoto wachanga wagonjwa na hasa wenye umri chini ya siku 28.

Wajuzi hao na wenzao wengi wanaopatikana sasa, ndio wamewezesha hata kufanyika utalii tiba, wageni kuja nchi kusaka tiba na wao wakialikwa nchi jirani kutoa msaada.

### MRADI MIUNDOMBINU

Sura ya pili ya uwekezaji iko katika miundombinu, dira ikijikita katika majengo, vifaa tiba, pamoja na dawa husika, kukabili shida za afya mahitaji ya tiba.

Rekodi hadi miezi saba iliyopita, inaonyesha katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake hadi kufika mwezi Machi mwaka huu, Rais Dk. Samia, kawekeza majengo 1,061.

**INAENDELEA UK.13**

MAZINGIRA

UKOMBOZI NA USALAMA BAHARINI...

# Wapewa mbadala uchumi, wafanikiwa kunusuru mazalia ya samaki ufukweni

**Na Boniface Gideon,** TANGA

KUSHAMIRI shughuli zitokanazo na kuongezeka watu jirani na ufukweni, kunatafsiriwa kusababisha ongezeko la shughuli za kibinadamu, hata kuchangia kupungua uzalishaji samaki mahali hapo baharini.

Ndani yake, kikubwa zaidi ni uharibifu wa makazi ya samaki maarufu 'matumbawe' unaotokana na uvuvi haramu unaohusu ukataji miti ya mikoko na uchafuzi wa bahari ufukweni.

Madhara mojawapo, ni katika uzalishaji samaki kama vile pweza walioko hatarini kutoweka, kutokana na 'matumbawe.' Ni hali inayowalazimu wadau wa maendeleo kujitokeza kuunga mkono juhudi za serikali kuhakikisha Uchumi wa Buluu.

Aina ya uchumi unaotajwa kuleta matokeo chanya katika jamii hadi sasa, ni kuanzishwa kampeni zinazohamasisha wakazi waishio pwani, wahakikishe wanatunza rasilimali bahari ili kuongeza uzalishaji samaki mahali hapo.

Hapo ndipo mmoja wa wadau katika ushirikiano wa umma na serikali (PPP), Shirika la Mwambao Coastal Community Network Tanzania, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kimataifa kama nchi za Norway, Asasi ya Eco Fish chini ya Jumuiya ya Ulaya (EU), The Nature Conversery (TNC) kwa ujumla wanafadhili kijiji cha Kigombe, wilayani Muheza.

Kinachofanyika, wadau hao wawawezesha kiuchumi wakazi wanaoishi mwambao wa Bahari ya Hindi, wanaoziwezesha Jumuiya za Wavuvi na Mfuko wa Kutunza Bahari (MKUBA).

Mpaka sasa wana boti mbili za ulinzi zimeshatolewa katika vijiji vya Boma Mahandakini na Boma, pia ikisaidia kuongeza wigo wa doria za ulinzi kwa vijiji tisa vya kata za Boma na Moa, zilizoko mpakani.

Huko wanatoa elimu ya utunzaji rasilimali bahari na kuwawezesha kiuchumi, wakiwapatia mitaji na vitendea kazi vya kupunguza shughuli za kibinadamu zinazofanywa baharini, ili kuongeza ulinzi wa kukabili wahalifu baharini.

Wilaya za Mkinga, Jiji la Tanga, Muheza na Pangani hadi majirani zao visiwani Zanzibar, ndio wanufaika wakubwa kwa kuwa shughuli zao nyingi za kiuchumi zinategemea bahari.

Wakazi wa maeneo hayo wameanzisha mfuko wa kuhifadhi chombo cha baharini 'MKUBA', kinachowezesha kupata fedha, vitendea kazi kama boti na




Viongozi wa Shirika la Mwambao Coastal Community Network Tanzania, wakikabidhi fedha kwa wanachama wa vikundi vya Mkuba wilayani Mkinga vinavyotetea usalama wa bahari, Tanga hivi karibuni. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

elimu ya utunzaji rasilimali za bahari, kupitia vikundi tajwa.

### BAHARINI KULIVYO

Mratibu wa Shirika la Mwambao Coastal Community Network Tanzania Mkoa wa Tanga, Ahmad Salim Omar, anasema hali ya bahari ni mbaya.

Anaorodhesha sababu zinajumuisha matukio ya uvuvi haramu, uharibifu wa makazi ya samaki, miti aina ya mikoko inazidi kukatwa kutokana na kuongezeka kwa matumizi yake katika jamii, uchafuzi wa fukwe za Bahari unaosababishwa na utupaji wa taka ngumu ambazo hugeuka kuwa sumu kwa viumbe bahari nalo ni janga jingine.

Hivyo kwa kuliona hilo, anasema wamelazimika kujitoa katika elimu ya utunzaji rasilimali za bahari na wakaunda mfuko maalumu wa kuhifadhi bahari unaoitwa MKUBA. Anasema, lengo la kuanzishwa mfuko huo ni kuwawezesha kiuchumi kwa kuwapatia mitaji na vitendea kazi wananchi wanaojiunga kwenye vikundi vya MKUBA wakiwapatia elimu ya utunzaji rasilimali za bahari na ujasiriamali wake.

"Kupitia mfuko huu, wanachama wanapata elimu ya utunzaji rasilimali za bahari, elimu ya matumizi ya fedha na ujasiriamali, lakini mwisho kabisa tunawawezesha fedha na vitendea kazi.

"Lengo ni kuhamasisha jamii ya ukanda huu wa bahari wanapunguza shughuli za kibinadamu baharini, ili kuruhusu samaki wanazaliane kwa wingi," anasema Ahmad.

Vilevile na ufafanuzi kwamba, wana kampeni ya kuhamasisha



Boti la doria lililokabidhiwa kwa ajili ya usalama wa baharini, wilayani Mkinga, Tanga. **PICHA: MTANDAO**

uchumi wa buluu, kupitia chombo hicho cha MKUBA na tayari anasema umeshaonyesha matokeo chanya, kwa zaidi ya wanufaika wake 4,422.

Kwa mujibu wa Ahmad, mfuko huo wa s8 wa Kutunza Bahari 'MKUBA' wamenufaika kupitia fedha zinazotolewa kupitia vikundi 148 ambavyo vipo kwenye mradi huo huku zaidi ya Sh.248 zikitumika kuwainua kiuchumi wanachama wa vikundi vya 'MKUBA'.

"Lengo letu ni kuhakikisha wakazi wanaoishi Mwambao wa Bahari,wanapata elimu ya utunzaji wa rasilimali za bahari na kuwainua kiuchumi ili wapunguze shughuli za kiuchumi huko baharini, na kwa kufanikisha hili tumeamua kuwawezesha fedha kupitia vikundi.

Anasema wilaya ya Mkinga imepewa kipaumbele zaidi kutokana na kuwa na shughuli nyingi za kiuchumi zinategemea bahari, pia ipo mpakani na nchi zingine.

"Halmashauri hii ya Mkinga tuna vijiji 12 kwenye programu za mradi huu wa MKUBA... pia kuna mradi mwingine unafadhiliwa na Ujerumani nao utakuja kwenye vijiji vingine," anasema Ahmad.

Anafafanua kuwa, wakazi wanaoishi mwambao wa baharini kutunza rasilimali za bahari, ili kuongeza uzalishaji wa samaki na kipato cha mwananchi mmoja mmoja.

"Niwaombe wananchi wenzangu mtunze rasilimali za bahari, msikate miti hasa ya mikoko na kwa wavuvi msitumie baruti na sumu, ni hatari kwa afya zetu walaji na viumbe hai wa majini.

"Pia, tujitahidi kufanya usafi kwenye fukwe, ili tuifanye bahari kuwa safi muda wote. Tukifanya hivyo, itatusaidia kuongeza uzalishaji samaki," anaongeza Ahmad.

### WANUFAIKA WANAFUNGUKA

Kassim Halfani, Mwenyekiti wa Jumuiya za Usimamizi wa Fukwe za Bahari (BMU) Wilaya ya Mkinga, anasema ujio wa mradi wa Mkuba umeongeza makusanyo ya ushuru kwa jumuiya hiyo na Halmashauri ya Mkinga.

"Tokea umekuja mradi huu, mazao ya samaki yameongezeka, wavuvi wamekuwa wanavua samaki wengi na hasa pweza.

"Mvuvi mmoja kwa sasa anavua zaidi ya kilo 50 ya pweza na kilo ya pweza ni kati ya shilingi 7,500 na 7,000, wakati hapo awali mvuvi mmoja alikuwa anavua kilo mbili. Haya ni mapinduzi makubwa sana kwetu na tunajivunia kwa hilo," anatamka Kassim.

Mwingine, Mohamed Ally, mkazi na mnufaika wa Mkuba, ana maelezo kwamba ni mageuzi yanayowafanya kuongeza uzalishaji samaki akiwa na ufafanuzi wake:

"Kinamama, vijana na wazee wote wamepata mitaji na wanafanya biashara.

Kiukweli imesaidia sana kuondoa wingi wa watu wanaofanya shughuli zao baharini, pia wengi wetu tulikuwa tunafanya kazi za uvuvi, ili tupate hela ya kula.

"Kwa sasa, tunafanya kazi za kutuingizia kipato cha familia, kinachoweza kuleta maendeleo ya familia, ikiwamo kujenga nyumba nzuri ya kisasa," anatamka Ally

### KUTOKA HALMASHAURI

Ofisa Uvuvi wa Halmshauri ya Wilaya ya Mkinga, Ezra Katete, anasema awali kabla ya mradi huo, hali ilikuwa ngumu zaidi hususani kwenye ulinzi na doria za baharini.

"Mdani ya muda mfupi baada ya ujio wa mradi huu, umeleta matokeo makubwa. Tumefanikiwa kupata boti za ulinzi na kwa kushirikiana na Jeshi la KMKM (Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo) tumeimarisha ulinzi baharini na kupambana na wavuvi haramu...

"Tayari tumeshakamata baadhi yao, lengo tunataka tuone matokeo chanya kwa jamii yetu inayoishi ukanda wa bahari," anasema Ofisa Uvuvi Ezra.

Anasifu juhudi za kutunza rasilimali za bahari na kuwainua wananchi kiuchumi zinazoendelea kuiunga mkono serikali katika kufikia uchumi wa buluu.

MAZINGIRA

# Wanasayansi wafukua undani Tsunami 2014 baharini, hadi enzi dunia changa

**Na Mwandishi Wetu**

HALI ya hewa iligunduliwa kwa mara ya kwanza mwaka 2014, ikisababisha wimbi la baharini liitwalo Tsunami, kubwa zaidi katika historia ya binadamu na kusababisha kuchemka bahari.

Kimsingi, Tsunami ni wimbi kubwa la baharini linalosababishwa na tetemeko la ardhi, mlipuko wa volkano au matokeo mengine yanayoleta mshtuko wa ghafla chini ya maji.

Mshtuko huo unasababisha kutokea wimbi kali linaloanza kupaa juu kufikia maji yaliko, hadi ufukweni mwa bahari.

Wanasayansi wamegundua mwamba wa anga za juu wenye ukubwa mara 200 kuliko ulioangamiza dunia wakati sayari dunia ilipokuwa changa miaka bilioni tatu iliyopita.

Wakiwa wamejihami kwa nyundo, wanasayansi walisafiri hadi eneo lenye athari Afrika Kusini, ili kutoa vipande vya mwamba vitakavyowasaidia kuelewa vizuri jambo hilo.

Timu hiyo pia ilipata ushahidi wa athari kubwa za miamba midogo inayoleta uharibifu duniani.

"Tunajua kwamba baada ya dunia kuundwa, bado kulikuwa na vifusi vingi vinavyopasuka angani ambavyo vilikuwa vikianguka duniani," anasema Profesa Nadja Drabon wa Chuo Kikuu cha Harvard, Uingereza.



Kikosi cha utafiti wa kisayansi kilichosafiri hadi ukanda wa Greenstone, Mashariki mwa Afrika Kusini kukusanya sampuli za mwamba, unaosadikiwa kuwa chanzo husika. **PICHA: MTANDAO**

"Sasa tumegundua maisha yalikuwa magumu baada ya baadhi ya athari hizi kubwa, lakini kulikuwapo ustawi na kufanikiwa," anasema.

Miamba anayoiita S2, ilikuwa mikubwa kuliko miamba ya anga za juu inayofahamika zaidi. Hiyo S2 ilikuwa kati ya kilomita 40 na 60 na uzito kati ya mara 50 na 200 zaidi. Ulianguka wakati dunia ilipokua bado katika miaka yake ya awali na ulionekana tofauti sana. Ilikuwa dunia ya maji na mabara machache tu yaliyotoka baharini. Maisha yalikuwa rahisi sana, viumbe waliundwa na seli moja.

Profesa Drabon alisafiri huko mara tatu na wenzake, akiendesha gari hadi milima ya mbali penye athari, wakiandamana na walinzi wenye bunduki kuwalinda dhidi ya wanyamapori kama vile tembo au faru, au hata majangili katika hifadhi ya taifa.

Walikuwa wakitafuta chembe au vipande vidogo vya mwamba vilivyoachwa kutokana na athari ya mwamba huo. Kwa kutumia nyundo, walichunguza mamia ya miamba na kuipeleka kwenye maabara kuchambua; Profesa Drabon alipakia vipande vya miamba.

**UVUMBUZI MKUU**

Timu hiyo sasa inaelezea upya hali ya hewa ya miamba ya S2 iliyosababisha dunia kuathiriwa. Iliunda mwamba wa kilomita 500 na iliyokatwa, kuondolewa kwa kasi kubwa sana, kuunda wingu lililozunguka dunia.

"Fikiria wingu la mvua, lakini badala ya matone ya maji, ni matone ya mwamba ulioyeyuka unaoanguka kutoka angani," Profesa Drabon anasema.

Mtaalamu huyo na timu yake wanasema, waligundua baadaye ushahidi kutoka kwenye miamba ulioonyesha mengi yaliyochochea kuwapo virutubisho kama madini ya fosforasi na chuma.

Anaeleza, Tsunami iliyozunguka sayari nzima, pia ilileta maji yenye utajiri wa chuma kwenye uso wa dunia na kutoa vimelea na nishati ya ziada.

Kwa mujibu wa Profesa Drabon, matokeo hayo yanaongeza mtazamo kati ya wanasayansi kwamba maisha ya zamani yalisaidiwa na vurugu katika miamba ambayo ilikuwapo duniani wakati huo.

"Inaonekana kwamba maisha baada ya athari yalipata hali nzuri sana ambayo iliruhusu kustawi," anaelezea na matokeo hayo yalichapishwa katika jarida la kisayansi la PNAS.

• ***Kwa mujibu wa BBC.***

# Fahamu silaha kuu za Awamu Sita zinazoibua mapinduzi ya afya nchini

**INATOKA UK.11**

Hiyo inagusa kutoka majengo 8549, hadi 9,610 huku mpango MMAM kwenye miaka 16 tangu uanze kutumika, ukielekeza kila kijiji au kitongoji kuwa na zahanati, kata kuwa na kituo cha afya, wilaya inakuwa na hospitali yake.

Pia hivi karibuni kukawapo uwekezaji wa fedha shilingi trilioni 1.02 katika ukarabati wa majengo ya zamani na kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la wagonjwa, binafsi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

**UHALISI UNAOENDELEA**

Kunatajwa ukamilishaji awamu za hospitali ya Kanda ya Kusini Mtwara na Hospitali ya Kanda Chato, ikiendana na upanuzi wa miundombinu kwa kujenga majengo mapya katika hospitali za rufani kanda (usimikaji mitambo ya kutibu saratani na mambo mengineyo); Kaskazini KCMC; Kanda Mbeya; Benjamin Mkapa- Dodoma na Bugando (Mwanza).

Pia hospitalini Sekou Toure (Mwanza); Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (Dodoma), Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto, Moshi.

Ni mpango unaozifikia hospitali mpya za rufani katika Mikoa ya Katavi, Njombe, Songwe, Simiyu na Geita.

Pia, kuna ya kuhamisha hospitali tano kutoka majengo yake ya zamani hadi mpya za kisasa kwenye mikoa ya Ruvuma, Shinyanga, Singida, Mara na Lindi, Rukwa, Kitete (Tabora) na Ukerewe (Mwanza).

Katika ngazi za msingi, rekodi ya Wizara ya Afya zinataja hospitali mpya za halmashauri 127 zimejengwa, kati yake 95 zimeanza kutoa huduma kwa wagonjwa tangu mwanzo wa mwaka na kuna ukarabati umefanyika kwa hospitali kongwe, kama vile Bombo ya jijini Tanga.

Ni takwimu inayofikia ujenzi wa vituo vya afya 367. Pia, hadi mapema mwaka huu, kuna maboma ya majengo ya zahanati 980 yamejengwa hata kuchangia ongezeko la vituo vya kutoa huduma za afya nchini.

Jedwali la kiserikali linafafanua kwamba, asilimia 80 ya wananchi wanapata huduma za afya ndani ya umbali wa kilometa tano ya maeneo wanakoishi, lengo kufikia asilimia 95 ifikapo mwaka 2030.

Hospitali tano nchini nazo zimehama kutoka majengo yake ya zamani, hadi mapya ambazo ni za rufani katika mikoa ya: Ruvuma, Shinyanga, Singida, Mara na Lindi.

Katika sura ya juu kuna hospitali za rufani ngazi ya mkoa, kanda, hospitali maalum kama vile za moyo na afya ya akili na MOI, juu kabisa kunakuwapo Hospitali ya Taifa ambayo ni Muhimbili (MNH).

Mgawanyo ulioko na asilimia wa uwiano kwa jumla kuu katika mabano; zahanati 7,999 (83.2%); vituo vya afya 1,170 (12.3%); hospitali wilaya 181(1.9%); hospitali rufani za mkoa 28(0.3%); hospitali zenye hadhi sawa na mkoa 36 (0.4%); hospitali za hadhi ya kanda 12 (0.1%); hospitali maalum sita (0.1%); na hospitali ya taifa iko moja (0.01%).

Ni aina ya tafsiri fulani ya matumizi ya pesa, inayotokana na jumla ya shilingi trilioni sita kuwekezwa katika Sekta ya Afya.

**HALI YA VIFAA**

Ndani ya uwekezaji kiafya unaoendelea nchini, Rais Dk. Samia, amwekeza pia katika vifaa kukiwapo shilingi bilioni 14.9 zilizozinduliwa na aliyekuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kusaidia ununuzi wa vifaa tiba kwa majimbo na halmashauri 214 nchi nzima.

Mtazamo mkuu wa Rais Dk. Samia, pia unagusa kumaliza vifo vinavyosababishwa na uzazi, hiyo ikiwa sehemu ya uwekezaji katika sekta ya afya.

Pia Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu, anampongeza Rais kutoa magari ya kubebea wagonjwa kwa wabunge wote 528, lengo ni kuboresha sekta ya afya nchini, hiyo ilikuwa hadi Novemba mwaka jana.

"Rais Samia ametoa magari hayo kwa wabunge kwa lengo likiwa kuhakikisha vifo vya mama na watoto vinapungua," anatamka Naibu Spika Zungu.

Mwaka huu, Waziri wa Afya, Jenista Mhagama ameipongeza Bohari ya Dawa MSD), kuendelea kuhakikisha inanunua vifaa vinavyohitajika kusaidia kuokoa maisha ya watoto wanaozaliwa njiti.

Ni kauli yake katika hafla kukabidhi vifaa tiba maalumu vya kuwasaidia watoto wenye matatizo ya kupumua, kwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Mohammed Mang'una kwa niaba ya waganga wakuu wote nchini.

Ni vifaa tiba 130 vyenye thamani ya Sh. 212,854,365, vilivyonunuliwa na MSD, kutekeleza agizo la Rais kusaidia kupunguza vifo vya watoto njiti, waziri akisisitiza ununuzi huo uwe endelevu.

AFYA

VITA ISRAEL NA PALESTINA WIKI HII...

# Simulizi na ushuhuda uliotawaliwa na vifo, majeruhi, saikolojia mateso

**Na Mwandishi Wetu**



Watoto waathitrika wa vita vya Israel na Palestina. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

HADI sasa simulizi hazipendezi katika makazi ya jamii ya Kipalestina, watu wanakimbia mashambulizi ya ardhini ya Israel kwenye kambi ya wakimbizi ya Jabalia, Kaskazini mwa Gaza, kukiwapo kundi la majeruhi na maiti zinazotapakaa njiani.

Ndio uhalisia wake mahali hapo, simulizi zikianza kwa mwanaume anayeeleza kwamba, kuna maiti zimetapakaa, baada ya kuamriwa kuondoka eneo hilo na wanajeshi wa Israel.

Mwanamke mwingine naye ana hayo, kwamba watu waliondoka kwa hofu kubwa na kuwaacha watoto wao, huku Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi wa Kipalestina, linatoa wito wa kusitishwa mapigano kwa muda, ili kuwezesha njia salama kwa familia zinazotaka kuondoka mahali hapo.

Hilo linachukua nafasi, huku hospitali mbili za ndani ya Palestina, zikitahadharisha kwamba zimeishiwa vifaa za kuwahudumia wagonjwa.

Israel inasema wanajeshi wake wanaendelea na operesheni dhidi ya wapiganaji wa Hamas, huku wakiwaondoa raia kwa usalama.

Zaidi ya watu 400 wanaripotiwa kuuawa na maelfu wameyakimbia makazi yao tangu jeshi lilipoanzisha mashambulizi ya tatu katika eneo la Jabalia mnamo Oktoba 6 mwaka huu, likisema linawatokemeza wapiganaji wa Hamas waliojipanga tena huko.

Operesheni hiyo imekuja wakati Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken akielekea Israel kujaribu kufufua mchakato wa kidiplomasia uliokwama kuhusu makubaliano ya kusitisha mapigano na kuwaachilia huru mateka kutoka Gaza.

Hiyo ni baada ya mauaji yaliyofanywa na wanajeshi wa Israel ya kiongozi wa Hamas Yahya Sinwar wiki iliyopita,Waziri wa Marekani Blinken, akisisitiza haja ya Israel kuchukua hatua za kuongeza mtiririko wa misaada ya kibinadamu kuingia Gaza, kuwasaidia raia wasiokuwa na makosa.

### USHUHUDA WA WANAOKIMBIA

Watu waliokimbia makazi yao katika kambi ya Jabalia na kutafuta hifadhi kitongoji cha karibu cha Rimal cha Gaza City, akiwamo mwanaume anayejitambulisha kwa jina la Saleh, ana maelezo kuu alikokuwa akiishi na familia yake.

Madaktari na wafanyakazi wa uokoaji, wanasema zaidi ya watu 20 waliuawa katika shambulio la anga la Israel eneo hilo, wiki moja iliyopita.

Jeshi la Israel limewataja wapiganaji 18 wa Hamas na Palestina Islamic Jihad siku ya Jumanne kuwa miongoni mwa waliofariki.

"Tulipokea ujumbe kupitia droni za Israel, zikitusihi tuhame, kwa hiyo tukaanza kutembea chini ya uangalizi wa wanajeshi wa Israel, ambao walitutaka tuelekee kusini au magharibi mwa Gaza. Nilikuwa na nyanya (mama wa bibi) yangu, alikuwa hawawezi kutembea, kama wengine wengi," anasimulia.

Mwanaume mwingine, Mohammed al-Danani, anasimulia alivyokuwa katika shule hiyo na akashuhudia miili ya waliouawa barabarani. Pia, alikuwa katika eneo la bwawa mojawapo wakati droni zikitangaza amri ya watu kuelekea mji wa Beit Lahia, Kaskazini mwa kambi hiyo.

"Hali ilikuwa ngumu sana, hakuna mtu aliyejua pa kwenda. Watu wengine walilazimika kukimbia bila watoto wao na kuwaacha shuleni huku wakitoroka na wengine," anasema.

Siku ya Jumanne wiki hii, Jeshi la Israel lilitangaza kuwa wanajeshi wake wanaendelea na mapigano katika eneo la Jabalia, huku wakiwahamisha raia kutoka eneo la mapigano.

"Maelfu ya raia wamehamishwa. Makumi ya magaidi wamekamatwa kutoka miongoni mwa raia," lilisema jeshi la Israel kwenye chapisho hilo, ila X - likijumuisha video inayoonyesha umati wa watu wakitembea katika mitaa iliyoharibiwa.



Hali halisi ya waathirika wa shambulizi la vikosi vya Israel, ndani ya Gaza.

Jeshi pia linakiri, askari wake wamewaua Wapalestina 10 wakiwataja "walikuwa tishio katika shambulio moja la anga," ingawa hawakutoa maelezo zaidi.

Nalo Shirika la Hilali Nyekundu la Palestina, lilichapisha video inayoonyesha gari la wagonjwa likisafirisha miili ya watu kadhaa waliouawa kwa kushambuliwa na makombora katika mji wa Jabalia Jumatatu wiki hii.

Pia, kuna simulizi ya video nyingine iliyorekodiwa siku hiyo, ikionyesha jitihada za mkazi mmoja anayejaribu kusaidia umma, wakiwamo kinamama na watoto waliojeruhiwa na wengine kufariki kwenye kambi ya shule iitwayo Jabalia.

Mwanamke aitwaye Dawasah, ana simulizi ya namna alivyotoroka eneo hilo siku ya Jumanne wiki hii akisimulia hali ya usalama ni ndogo, kuwapo majeruhi na hapakuwapo gari la kubeba wagonjwa.

### KUTOKA UMOJA MATAIFA

Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA), Philippe Lazzarini, anasema wafanyakazi wake Kaskazini mwa Gaza wanaripoti hawakuweza kupata chakula, maji au huduma za matibabu.

"Harufu ya maiti ipo kila mahali kwani miili imeachwa imelala barabarani au chini ya vifusi," Lazzarini aliandika kwenye mtandao 'X' na kuongeza: "Watu wanangojea tu kufa. Wanajihisi kutelekezwa, kutengwa, na hawana tumaini."

Lazzarini ana wito akinena: "Kusitishwe mapigano mara moja, hata ikiwa kwa saa chache, ili kuwezesha njia salama za kibinadamu kwa familia zinazotaka kuondoka eneo hilo na kufika maeneo salama."

Kutoka Umoja wa Mataifa, kuna ufafanuzi kwamba serikali ya Israel inaendelea kukataa ombi la ofisi yake ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA), kusaidia kuwaokoa raia waliokwama chini ya vifusi na kuwasilisha vifaa vinavyohitajika katika hospitali.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Indonesia, ambayo ni mojawapo ya wanaofanya kazi karibu na Jabalia, Dk. Marwan al-Sultan, akisema wanajeshi wa Israel, walisimama nje ya lango na kulikuwa na milio ya risasi kila mara eneo hilo.

"Hilo limezua hali ya hofu na kuchanganyikiwa kwa wagonjwa na wafanyakazi wa matibabu," anasimulia Dk. Marwan al-Sultan, akiongeza: "Pia tunakabiliwa na uhaba mkubwa wa mafuta, vifaa vya matibabu, wafanyakazi, chakula na maji.

"Aidha, kukatika kwa umeme kunaendelea kulazimu hospitali kutegemea vyanzo vya nishati mbadala vinavyodumu kwa saa nane hadi 10 pekee na hilo linahatarisha usalama wa wagonjwa."

Hata hivyo, jeshi la Israel linakanusha kwa kusema linahakikisha hospitali zinafanya kazi wakati wa mashambulizi hayo, ikiwa na uthibitisho wake kwamba hilo lipo tangu wiki iliyopita.

Kwa mujibu wa taarifa ya jeshi hilo, ni kwamba zaidi ya malori 230 ya kubeba chakula, maji, vifaa vya matibabu na malazi yamepelekwa Kaskazini mwa Gaza, kupitia kivuko kilichoko Magharibi mwa eneo hilo.

Hiyo ni baada ya Umoja Mataifa kunena kwamba imepita wiki mbili sasa, jamii hiyo haijapatiwa mahitaji ya lazima wakati vita vikiendelea.

Israel ilianzisha operesheni ya kuiangamiza Hamas kujibu mashambulizi ya kundi hilo Kusini mwa Israel mnamo Oktoba 7, mwaka jana na takribani watu 1,200 waliuawa na wengine 251 walichukuliwa mateka.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya ya eneo hilo inayoendeshwa na Hamas, hadi sasa kuna zaidi ya watu 42,710 wameuawa huko Gaza, tangu operesheni hiyo ya Israel kuanza.

***• Kwa mujibu wa taarifa ya kimataifa.***



# Singida wavuna mabilioni sekta ya madini

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MKOA wa Singida umeongeza ukusanyaji mapato katika sekta ya madini kutoka Sh. bilioni 4.7 mwaka 2021 hadi kufikia Sh. bilioni 13.7 mwaka jana.

Mkuu wa Mkoa huo, Halima Dendego, alieleza hayo juzi kwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, akiwa kwenye ziara ya siku tano mkoani hapa kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Dendego, alisema uwekezaji katika sekta hiyo umeendelea kushika kasi katika mkoa huo na wachimbaji wadogo na wakubwa kuongezeka na kupatiwa leseni 821 za uchimbaji.

Vilevile, alisema mkoa umetenga hekta 6,000 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na kwamba kwa sasa una kiwanda kikubwa kimoja, vya kati 10, vidogo 309 na vidogo zaidi 1,483.

**"Kumekuwa na mwamko wa kujenga viwanda katika Mkoa wa Singida, hivi sasa kuna viwanda vitatu vikubwa ambavyo vitazinduliwa hivi karibuni ambavyo ni cha mafuta ya kula ya alizeti, sabuni**

"Kumekuwa na mwamko wa kujenga viwanda katika Mkoa wa Singida, hivi sasa kuna viwanda vitatu vikubwa ambavyo vitazinduliwa hivi karibuni ambavyo ni cha mafuta ya kula ya alizeti, sabuni na juisi," alisema.

Kuhusu umeme, alisema hivi sasa vijijj vyote 441 vimefikishiwa nishati hiyo na hatua inayofuata kupelekwa kwenye vitongoji.

Aliongeza kuwa maendeleo makubwa yamefanyika katika mkoa huu kutokana na kupokea fedha nyingi kutoka serikali.

Dendego, alisema bajeti ya mwaka wa fedha uliopita, zilipangwa kupelekwa Sh.bilioni 239 lakini walizopokea ni Sh.bilioni 241 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Waziri Silaa alipongeza maendeleo makubwa yaliyofanyika katika mkoa huo kwa ushirikiano.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, akizungumza juzi kwenye mkutano wa hadhara na wananchi wa Kijiji cha Hika, Kata ya Makuru, mkoani Singida baada ya kuzindua mnara wa mawasiliano ya simu uliojengwa na serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa Sh. milioni 272.
**PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# UDOM, Wamarekani kushirikiana kufundisha masomo ya sayansi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHUO Kikuu cha Dodoma (UDOM) na ujumbe kutoka Chuo Kikuu cha Idaho nchini Marekani wamefanya mazungumzo yenye lengo la kuanzisha ushirikiano katika ufundishaji wa masomo ya sayansi.

Akizungumza katika kikao chao jana jijini hapo, Naibu Makamu wa Chuo Mipango, Fedha na Utawala, Profesa Wineaster Anderson, alisema kuwa watashirikiana kufanya utafiti wa kisayansi, kubadilishana wanafunzi na wahadhiri ili kujifunza na kuongeza uelewa zaidi katika masomo hayo.

Alitaja maeneo mengine watakayoshirikiana kuwa kufanya miradi, kutoa huduma za upandikizaji figo, uroto na matibabu ya saratani.

"Miradi hii ipo katika hatua za mazungumzo ya uanzishwaji wake na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya Tanzania," alisema.

Prof. Luke Harmon kutoka Idaho, alisema watashirikiana kufundisha kwa vitendo, matumizi ya vifaa vya kisayansi na kufanya semina kusaidia kukuza uelewa kwa wanafunzi.

Awali, Mwakilishi wa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo - Taaluma, Tafiti na Ushauri Elekezi wa UDOM, Profesa Ainory Gesase, alisema watashirikiana kufanya utafiti wa magonjwa yanayoiathiri jamii kama kisukari na upatikanaji wa majisafi.

Profesa Gesase, alisema kuwa wahadhiri wakipatiwa maarifa ya kutosha, watafundisha wanafunzi kwa weledi.

Kaimu Amidi wa Shule Kuu ya Afya na Tiba ya Meno -UDOM, Dk. Jumanne Shakiru, alisema mazungumzo hayo yamekuja wakati mwafaka kutokana na chuo kuendelea kuboresha mitaala na kuanzisha programu mpya ya 'Biomedical Engineering'.

# Watoto watibiwa macho Benjamin Mkapa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH) kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Light for the World imeweka kambi ya wiki moja ya kutoa matibabu ya macho kwa watoto wadogo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Macho, Dk. Amon Mwakakonyole, alisema kuwa kambi hiyo iliyoanza juzi, itahusisha matatizo jumuishi ya macho yanayowaathiri watoto wadogo na kupatiwa matibabu. "Naomba jamii itumie kambi hii kuleta watoto kupata matibabu ya macho, kutakuwa na madaktari bingwa kutoka BMH na nje ya hospitali hiyo," alisema Dk. Mwakakonyole.

Aliyataja matatizo ya macho yanayowakumba zaidi watoto kuwa ni mtoto wa jicho na uoni hafifu ambayo husababishwa na magonjwa ikiwamo kisukari.

Alisema magonjwa hayo yanatibika, hivyo jamii inapaswa kuwahi hospitali kabla matatizo hayo hayajawa makubwa.

"Magonjwa ya uoni hafifu yanarekebishika kwa kuvaa miwani, wazazi na walezi wanapaswa kutumia nafasi ya kambi hii watoto kupata matibabu na kuendelea na masomo yao bila changamoto yoyote, " alisema Dk. Mwakakonyole na kuongeza kuwa watu wazima nao watapatiwa matatibu.

Alisema kambi hiyo inaambatana na uzinduzi rasmi wa matibabu ya macho katika hospitali hiyo, itakuwa ikihudumia mikoa ya Iringa, Manyara na Singida.

Daima Makassy, Mkazi wa jijini Dodoma, aliishukuru serikali kwa kuanzisha huduma za macho katika hospitali hiyo na kuwapunguzia gharama za kusafiri kwenda sehemu nyingine kupata matibabu ya macho.

"Tatizo la macho linachangamoto kubwa hususan kwa watoto, linasababisha mtoto ashindwe kufanya vizuri darasani kutokana na kuwa na uoni hafifu bila yeye kujua," alisema.





# Madereva 6,800 watiwa mbaroni

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi mkoani hapa, limewakamata madereva zaidi ya 6,800 kwa kukiuka sheria za usalama barabarani kwa kipindi cha mwezi Septemba mwaka huu.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Mahamoud Banga, juzi aliwaambia waandishi wa habari kuwa madereva hao walikamatwa katika msako uliofanywa kulingana na taarifa wanazopata kutoka kwa wananchi.

Banga, alisema baada ya madereva hao kufikishwa mahakamani, watatu walifungiwa leseni na 6,832 kutozwa faini.

Vilevile, alisema jeshi hilo limefanikiwa kuzuia ajali kwa kutoa elimu kwa madereva, wamiliki wa vyombo vya moto, shuleni na kwa wananchi.

**Kwa upande mwingine, alisema wamewakamata watu 30 kwa makosa mbalimbali, ikiwamo wizi wa pikipiki, uporaji, uvunjaji, utapeli kwa njia ...**

"Tumefanikiwa kupunguza makosa mbalimbali kwa kiasi kikubwa," alisema kamanda huyo.

Kwa upande mwingine, alisema wamewakamata watu 30 kwa makosa mbalimbali, ikiwamo wizi wa pikipiki, uporaji, uvunjaji, utapeli kwa njia ya mtandao, mauaji na ukiukwaji wa sheria.

Ameitoa wito kwa madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali na kusababisha watu kujeruhiwa, kupata ulemavu na wengine kufa.

Baadhi ya wakazi mkoani hapa, akiwamo John Sanga, alisema bado kuna madereva waendesha magari bila ya kuzingatia sheria za usalama barabarani.

"Tunaliomba Jeshi la Polisi liendelee kutoa elimu kwa madereva kwa sababu bado wamekuwa wakigharimu maisha ya watu," alisema Sanga.



Kamishna Msaidizi wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Janeth Hiza (kulia), akiwakaribisha machifu wa Jiji la Mbeya walipotembelea jana banda la wizara hiyo, katika Maadhimisho ya Nne ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa yanayoendelea Viwanja vya Ruanda-Nzovwe, jijini Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtaka akerwa utoro shuleni

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amekemea tabia ya utoro wa wanafunzi katika shule za sekondari na msingi kwa kuchochewa na wazazi na walezi kisha kuwatumikisha kwa shughuli za uchumi na kuwaingizia kipato cha kujikimu na maisha.

Mtaka alikemea tabia hiyo juzi wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Joseph Mbeyela iliyoko Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Mtaka, alisema licha ya serikali kuboresha miundombinu ya elimu kwa kujenga madarasa, matundu ya vyoo na kutengeneza samani, bado kuna wazazi na walezi hawatilii mkazo elimu.

Alisema inatia uchungu kuona wazazi bado wanashiriki kukwamisha watoto wao kwenda shule kwa kuwashawishi kufanya vibaya katika mitihani ya taifa ili wakose nafasi ya kuendelea na masomo.

"Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) alifanya maamuzi ya kujenga vyumba vya madarasa 15,000 nchi nzima kwa shilingi bilioni 300 ili watoto wa Tanzania wanapofungua shule siku moja form one wote waanze kidato cha kwanza, ni bahati mbaya sana pamoja na juhudi zote za serikali, kuna wanafunzi watoro shuleni," alisema Mtaka.

Aliwasisitiza wanafunzi hao changamoto ya ajira isisababishe wakaacha shule badala yake wasome kwa bidii kwa sababu serikali imeweka mazingira rafiki ya kusoma na kujifunza.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe ambaye ni Ofisa Mipango, John Malle, alisema halmashauri hiyo imepokea zaidi ya shilingi bilioni 6 kwa ujenzi wa madarasa takribani 170.

Baadhi ya wanafunzi wa kidato cha nne, akiwamo Samwel Kidava, aliishukuru serikali kwa kuboresha miundombinu katika sekta ya elimu na vifaa vya kujifunzia na kuahidi kufaulu mitihani hiyo.

Mkuu wa Shule hiyo, Jimmy Ngumbuke alisema wana sababu kuahidi kufanya vizuri katika mitihani ya taifa kutokana na maandalizi waliyoyafanya kwa wanafunzi wao.

Novemba 11, mwaka huu, wanafunzi wa kidato cha nne nchini, wanatarajia kufanya mitihani ya kuhitimu elimu ya sekondari nchini, wa kidato cha pili Oktoba 28.

# Wanafunzi wa kike kujengewa mabweni

**Na Agustino Kihombo,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Peter Serukamba, amesema serikali imedhamiria kujenga mabweni katika shule za sekondari mkoani hapa ili kuwaondolea adha watoto wa kike kutembea umbali mrefu na kukatisha masomo.

Mpango huo alitangaza juzi baada ya ziara ya kukagua miradi ya ujenzi wa mabweni katika shule za sekondari Kilosa, Mawelewele na Nduli.

Alisema hatua hiyo inalenga kuboresha mazingira ya elimu kwa wanafunzi wa kike, kuhakikisha wanapata mazingira salama ya kusoma na kuishi.

Serukamba, alisema ujenzi wa mabweni hayo utapunguza matatizo yanayowakabili wanafunzi hao kama umbali mrefu wa kusafiri kwenda shule na hatari wanazoweza kukumbana nazo njiani.

"Leo tumefanya ziara Manispaa ya Iringa kukagua miradi ya sekta ya elimu, tumekagua ujenzi wa mabweni, nimemwagiza mhandisi kuhakikisha unakamilika ifikapo Novemba 31, mwaka huu ili ikifika Januari wanafunzi waingie kwenye mabweni," alisema Serukamba.

Meya wa Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwada, alisema ni mpango wa halmashauri kuhakikisha wanafunzi wanapata mahali pa kuishi wawapo shule kwa kujenga mabweni na serikali kuweka kipaumbele kwa kutoa fedha katika miradi hiyo.

Ngwada, alisema baada ya ujenzi wa mabweni hayo, wamejipanga kuendelea na nyumba za walimu ili kuwapa nafasi kufanya kazi karibu na maeneo ya shule.

Baadhi ya wanafunzi, akiwamo Esther Samwel, alisema ukosefu wa mabweni umekuwa ukiathiri mwenendo wa taaluma kwa kutembea umbali wa kilometa zaidi ya 20 kwenda na kurudi shule, hivyo ujenzi wa mabweni hayo, utatatua kero hiyo, kuongeza ari ya kusoma na kuongeza ufaulu.

"Ukosefu wa mabweni ni changamoto kubwa kwetu kama wanafunzi tumekuwa tukipitia adha ya kuamka usiku saa tisa hadi kumi ili kuwahi shuleni, tukifika tunakuwa tumechoka hali inayotufanya tushindwe kufanya vizuri kwenye masomo yetu, ujenzi wa mabweni haya tunaishukuru serikali kwa kutupa kipaumbele ili tusome katika mazingira bora," alisema Esther.

# Mwamko waongezeka ukataji bima

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amesema mwamko wa wananchi kukata bima umeongezeka. Abdulla aliyasema hayo wakati akizungumza na uongozi wa kampuni zinazotoa huduma ya bima kutoka Tanzania Bara na Zanzibar ofisini kwake Vuga.

Alifafanuwa kuwa wananchi hao wameonyesha mwitikio huo baada ya kupatiwa umuhimu wa kukata bima kwa ajili ya matibabu na mali zao na kampuni hizo ikiwamo Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania (TIRA).

Alisema serikali kupitia mashirika ya bima imekuwa ikiwahamasisha wananchi na wawekezaji kukata bima ili kupunguza gharama ya majanga yanapotokea katika mali zao na taasisi.

Alisema serikali iko tayari kushirikiana na kufanya kazi na kampuni yote ya bima nchini kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na salama kwa mali zao na afya zao.

Makamu huyo wa pili wa rais amezitaka kampuni hizo kuwa karibu na wananchi kwa kuwapa elimu, faraja wanapopatwa na majanga na kutumia muda mfupi kuwalipa fidia ya mali zao badala ya kuwazungusha.

Kamishna Mkuu wa TIRA, Dk. Bhaghayo Saqware, alisema kwa kushirikiana na serikali, kampuni hizo zipo katika mchakato wa kuandaa sera ya Bima ya Taifa itakayotilia mkazo na kutoa miongozo kwa kila wizara kulinda mali, rasilimali na afya za watumishi.

Mwenyekiti wa Chama cha Kampuni zBima nchini, Florah Minja, alisema wataendelea kushirikiana na serikali ili kuhakikisha mwamko wa wananchi na taasisi unaongezeka katika ukataji wa bima.

# Saratani shingo ya kizazi bado janga nchini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake imechangia kwa kupunguza nguvu ya uchumi kwa wananchi visiwani hapa kutokana na waathirika kukosa afya na kutumia gharama kubwa ya kupata matibabu ndani na nje ya nchi.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Wizara hiyo, Dk. Amour Suleiman Muhamed, wakati wa uzinduzi wa uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi iliyofanyika katika Hospitali ya Wilaya ya Magharib B Mwanakwerekwe visiwani hapa.

Uchunguzi huo hufanyiwa kila mwaka na madaktari bingwa wa wizara hiyo kwa kushirikiana na wa kutoka nchini China.

Alisema gharama za kutibu saratani ni kubwa ikilinganishwa uchumi wa wananchi viswani hapa, hivyo kushindwa kumudu kwa kukosa fedha.

Alisema serikali hulazimika kuingia gharama ya kuwapatia matibabu wananchi wake waliopata athari hiyo na wengine kuwapeleka nje ya nchi ili kuokoa maisha yao.

Alisema kwa wastani kwa mwaka wagonjwa 60 kutoka Zanzibar hupelekwa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road jijini Dar eS salaam kupatiwa huduma ya mionzi na nyingine na kutumia kiasi cha Sh. milioni 60 kwa mwezi.

> **"Serikali inatumia gharama kubwa kuwahudumia wagonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi na kwa mwaka hugharamika shilingi milioni 900," alisema**

"Serikali inatumia gharama kubwa kuwahudumia wagonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi na kwa mwaka hugharamika shilingi milioni 900," alisema mkurugenzi huyo.

Alisema kutokana na changamoto hiyo, serikali imeweka utaratibu huo wa kufanya uchunguzi kwa wananchi wake ugonjwa huo ili watakaogundulika kuwa nao waanze kupatia matibabu mapema.

Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, alisema serikali inahakikisha inaboresha miundombinu ya afya kwa kujenga hospitali kila wilaya na kushirikiana na wataalamu kutoka nchi mbalimbali ikiwamo China kufanya uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi.

Takwimu zinaonyesha watu milioni 40 nchini kila mwaka wanagundulika kuwa na saratani, kati yao milioni 26 wanakufa kwa saratani ya shingo ya kizazi.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, asilimia 25 inayofuatiwa ni wale waliogundulika kuwa na saratani ya matiti kwa wanawake na tezi dume kwa wanaume.

Takwimu hizo zinaonesha uwezekano wa kupata saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake ni asilimia 16 kabla ya kufika miaka 75.




Washiriki wa kongamano la kumpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kutimiza miaka minne ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nane, lililoandaliwa na Jumuiya ya Wazazi Tanzania, Wilaya ya Mjini Unguja, wakifuatilia hotuba ya ufunguzi wa kongamano hilo, wakati Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar akihutubia juzi. **PICHA: IKULU**

# Chanzo umaskini wanawake vijijini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, amesema wanawake vijijini wanakabiliwa na mzigo wa kulea watoto hadi kushindwa kufikia malengo ya kuondokana na umaskini katika familia zao.

Mohamoud alitoa kauli hiyo wakati akikabidhi vifaa kwa wajasiriamali wakiwamo wakulima wa mwani wa mkoa huo vilivyotolewa na Jukwaa la Wanawake Afrika (FAWE) kupitia mradi wa kuwasaidia wanawake kwenye uchumi.

Alisema hali hiyo imechangia wanawake hao kushindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli zao za kiuchumi kutokana na kuelemewa na kazi kubwa ya kulea watoto na kuzidi kuwa maskini.

Alilipongeza Shirika la Kimataifa la Kusaidia Maendeleo ya Wanawake (UN WOMEN) kwa kushirikiana na (FAWE) kujenga makazi ya kulea watoto wakati mama zao wakiwa katika shughuli za kiuchumi, ikiwamo kilimo cha mwani katika Kijiji cha Muungoni na Uzi.

Mahamoud, alisema vituo hivyo vinapaswa kuwapo katika vijiji vingine vya mkoa huo kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa wanawake. Alisema anatarajia baada ya wanawake hao kukabilidhiwa vifaa hivyo, watakwenda kuvitumia kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuwaingizia kipato.

Alisema wakazi wa mkoa huo asilimia 55 wanategemea kilimo kwa ajili ya kupata chakula, hivyo kuguswa kwa kundi hilo kutasaidia kuimarika kiuchumi.

"Unapomwezesha mwanamke umeiwezesha familia, kwa hivyo kuguswa kwenu kwenye mradi huu maana yake tumeiwezesha jamii ya mkoa huu," alisema Mahamoud. Alisema dhana ya uwekezaji imegusa nyanja mbalimbali, ikiwamo uongozi, kuanzisha vikundi kwa ajili ya kupata mikopo na kutumika mitaji ya kuendeleza biashara zao.

Akizungumzia changamoto ya bei ya mwani, alisema zipo hatua ambazo serikali imeanza kuchukua ikiwamo ujenzi wa kiwanda cha kuchakata zao hilo.

Mahamoud, alisema katika mkoa huo, kuna mradi maalum kwa ajili ya kujenga kituo cha kuhifadhi na kuchakata mwani.

Alisema kiwanda hicho kinajengwa kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB).

Mratibu wa FAWE, Winnifred Yatuwa Mamawi, alitaja changamoto zinazowakabili wakulima wa mwani kuwa ni pamoja na bei ndogo, ukosefu wa vifaa na kushindwa kufika katika kina kirefu cha maji ya Bahari ya Hindi unakolimwa baada ya kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Winnifred, alisema kupitia mradi wa kuwasaidia wanawake kiuchumi, wametoa elimu kukabiliana na changamoto hizo, ikiwamo kuanzisha vikundi vya akiba na mikopo, kujenga vituo vya malezi ya watoto.

Wakizungumza baada ya kupokea vifaa hivyo, wanufaika hao waliahidi kutumia kwa malengo waliyopewa ili kuinua kipato na kuboresha maisha yao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SERAPHINA WILLIAM NGOLE** ANATANGAZA KUPOTEA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX-NO **S0430-0090** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA UWEMBA SEKONDARI MWAKA 2012. YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **NJ/RB/4339/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DHUKAELAR KAESSAR SAGAR** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba **S2348/0003** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ILALA ISLAMIC SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/227908/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARTIN N. NKOLLO** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba **S.1049/0092** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. THOMAS AQWINAS SEC. SCHOOL** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/228533/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DOMINIC MWAKASEGE** anatangaza kupotea kwa cheti cha UALIMU chenye namba **E0523-0081** kilichotolewa na **MONDULI TEACHERS' COLLEGE** mwaka 2023. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MOR/KIL/15788/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MERCY MZIRAY NYANGE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 589 BHV – TOYOTA LANDCRUISER PRADO.** Chassis namba **KDJ950017593.** Engine namba **IKD0822749.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/193788/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FATUMA MAHUNGO MRUTU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 183 CLC – TOYOTA RAUM.** Chassis namba **NC2200002454.** Engine namba **INZA768341.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/224987/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**SALIM MRISHO NGASA** anatangaza kupotea kwa kadi za Pikipiki zenye namba za usajili **MC 218 DEB, MC 400 DGA, MC 279 DAH, MC 188 CNH na MC 675 DKV.** Yeyote atakayezionа atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/227675/2024.**

---

**MAHAKAMA YA WILAYA YA SINGIDA**
**MKOA WA SINGIDA**

**HATI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI Na. 25810/2024**

**OMBI LA ELIZABETH SAMSON IDABU kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu CHARLES ABEDI MSONIA KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote wa mirathi ya marehemu **CHARLES ABEDI MSONIA** wanaalikwa kuja Mahakamani kuhudhuria kesi wakiwa wanataka mnamo tarehe 18 mwezi Novemba mwaka 2024 kabla mwombaji huyo hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo.

Tarehe **16/10/2024**

**Hakimu mkazi**
**Mahakama ya Wilaya -Singida**

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 20082 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE BETWEL RAPHAEL CHOVE**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY COLLIN BETWEL CHOVE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 17 day of 10...2024

Dated at DAR ES SALAAM this 21 day of 08...2024.

Senior Resident Magistrate

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI** **Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na.43/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ENOCK ELIAS NTANGEKI wa MAILIMBILI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ANGELA KAMGISHA ISSA**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 Mwezi 11 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 22 Mwezi 10 Mwaka 2024

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI NA. 216 YA MWAKA 2024**

**ALLEN HILLARY CHAMI..........................................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**CHRISTINA MASAGASI..................................MJIBU MAOMBI 1**
**YOHANA ALEX BUNDALA.............................MJIBU MAOMBI 2**

**KWA:**
**CHRISTINA MASAASI NA**
**YOHANA ALEX BUNDARA**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 27.11.2024 saa 3:00 asubuhi.
**ANGALIZO:** Kama hautahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/ Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 23 ya mwezi wa OCTOBA, 2024.

MWENYEKITI.
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.
DODOMA.

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOROGORO SUB – REGISTRY**
**AT MOROGORO**

**LAND APPEAL NO. 25037 OF 2024**

**TERESIA AUGUSTINO...........................................APPELLANT**

**VERSUS**

**FIDELIS LIBERAT SHAYO & 2 OTHERS............RESPONDENTS**

**NOTICE TO APPEAR**
**SUBSTITUTED SERVICE**
**Made under Section Order 5 Rule 20 (1) of the Civil Procedure Code 20, Cap. 33 R. E 2022]**

**TO:**
**1. DANIEL MPOMA**
**TAKE NOTICE** that the above named Appellant has instituted a suit against you and the same is fixed for HEARING on 29TH day October, 2024 at 09:00 A.M, before Hon. H. Kinyaka, J. in the High Court of Tanzania at Morogoro.
YOU are thus required to appear in person or through your Advocate or dully authorized agent without fail.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on the aforementioned date and time, the Court shall proceed to hear and determine the case in your absence.
**GIVEN under my HAND and SEAL** of this COURT this 21st October, 2024.

**DEPUTY REGISTRAR**
**MOROGORO**

---

**FORM NO. A/1**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE HIGH COURT OF SONGEA**
**AT SONGEA**

**CIVIL CASE NO 16285 OF 2024**

**REGINA ELITERIUS NDONDE............PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**NGAHOKOLA VILLAGE AND OTHERS................DEFENDANT(S)**

**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V.r 1 Civil Procedure Code)**

**TO: JULIUS NYONI**

**WHEREAS** the above named Plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;
**YOU ARE HEREBY NOTIFIED** that you must file your **WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE** in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
**AND TAKE NOTICE** that if you default in filing of the written statements of defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.
**TAKE FURTHER NOTICE** that the case also has been fixed for order before **Hon. E.L KAWISHE** Judge/Magistrate on the 23 day of 10, 2024 at 9:00 O'clock in the forenoon/afternoon.
**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 14 day of 8, 2024.**

REGISTRAR/MAGISTRATE

---


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Trump alalamikia Labour kusaidia kampeni za Kamala Harris

**WASHINGTON,** Marekani

KAMBI ya Kampeni ya rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump, imewasilisha malalamiko kwa Tume ya Uchaguzi ya Shirikisho (FEC), ikidai Chama cha Labour cha Uingereza, kinaingilia uchaguzi kwa kumsaidia Kamala Harris.

Katika malalamiko hayo yanataja ripoti za vyombo vya habari kuhusu mawasiliano kati ya Chama cha Labour na kambi ya kampeni ya Harris pamoja na misaada ya kujitolea inayotolewa kwa Chama cha Democrat.

Ilieleza misaada hiyo sawa na michango isiyo halali.

Hata hivyo, BBC ilielewa kuwa wanaharakati wa Chama cha Labour wanaofanya kampeni katika uchaguzi wa rais wa Marekani wapo kama watu binafsi.

Hata hivyo, Chama cha Labour hakijatoa jibu rasmi kuhusu tuhuma hizo.

Malalamiko hayo yanataja gazeti moja ambalo liliripoti kuwa watu wanaohusishwa na Chama cha Labour wamesafiri hadi Marekani kumfanyia kampeni Harris.

Wanadai huo ni uingiliaji wa wazi wa Chama cha Labour, na kambi ya kampeni ya Harris imekubali michango isiyo halali kutoka nje ya nchi.



Kamala



Trump

# Nchi za BRICS kuanzisha mfumo mpya wa kifedha

**MOSCOW,** Russia

VIONGOZI wa mataifa yanayounda jumuiya ya BRICS, wanatarajia kupitisha azimio la ushirikiano wa kifedha unaokwepa mfumo wa Swift unaoongozwa na Marekani.

Mkutano huo ulioanza Jumanne unawakutanisha viongozi waanzilishi wa mataifa matano ya Brazil, Afrika Kusini, China, India na Russia.

Rais Vladimir Putin alieleza katika mkutano huo ajenda kuu ni kuanzisha mfumo mbadala wa kifedha ili kuleta ushindani na wa SWIFT, ambao miamala yake ya kimataifa inadhibitiwa na mataifa ya magharibi.

Benki nyingi za Russia ziliondolewa kwenye mfumo huo kama moja ya utekelezaji wa vikwazo kutokana na kuivamia Ukraine.

Mshauri wa Mambo ya Nje wa Russia, Yuri Ushakov, aliutaja mkutano huo kuwa ni tukio kubwa zaidi la kidiplomasia kuwahi kuandaliwa na nchi hiyo. Nchi nyingine 36 zinahudhuria mkutano huo wa BRICS, wakiwamo wakuu wa nchi 20.

Rais wa China Xi Jinping alifanya mazungumzo ya faragha na Rais Putin, kujadili kuhusu mgogoro wa Ukraine pamoja na mahusiano kati ya nchi wanachama wa BRICS.

Rais Xi alimwambia Putin kuwa ulimwengu uko katika hali ya sintofahamu lakini urafiki wao wa kimkakati utaendelea kudumu hadi kwa vizazi vijavyo.

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, alisema nchi yake inathamini uhusiano wa dhati na Russia na kusisitiza Rais Putin ni rafiki na mshirika wa kweli kwa nchi yake tangu zama za vita dhidi ya ubaguzi wa rangi.

Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi alimwambia Rais Putin, kuwa vita vya Ukraine vinapaswa kumalizwa kwa njia ya amani na kwamba India iko tayari kutoa msaada wowote utakaohitajika.

Rais wa Brazil, Luiz Inacio Lula Da Silva, ambaye hakuhudhuria mkutano huo wa BRICS baada ya kuumia kutokana na ajali aliyopata akiwa kwenye makazi yake, atashiriki katika mkutano huo kwa njia ya video.

Baada ya chakula cha jioni, Rais Vladimir Putin alikutana kwa mazungumzo na Rais wa Misri Abdelfattah al-Sisi ambaye alipongeza uungaji mkono wa Russia kwa miradi ya kiuchumi ya Misri, ikiwamo kinu cha nyuklia cha Dabaa kwenye pwani ya Mediterania. **DW**



Lori la mafuta likiwaka moto baada ya kupinduka katika kitongoji cha Kigoogwa nje ya Jiji la Kampala, Uganda jana. Watu 10 walikufa wakati wakijaribu kuchota mafuta. **PICHA: AP**

# Kitendawili sakata la Gachagua, Ruto afungua kesi

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, William Ruto amefungua kesi Mahakama Kuu akiomba kesi kadhaa zilizowasilishwa mahakamani hapo zinazopinga kuondolewa madarakani makamu wake, Rigathi Gachagua, kutupwa.

Katika nyaraka zilizowasilishwa mahakamani hapo jana, Rais Ruto, alidai masuala yaliyoibuliwa katika kesi hizo yanaweza kusikilizwa na Mahakama ya Juu pekee.

Hata hivyo, jana Gachagua ambaye aliondolewa madarakani baada ya kupigiwa kura na wabunge na seneti, alihudhuria kikao cha kwanza cha Mahakama Kuu wakati wa kusikilizwa kwa kesi mbili za kupinga kuondolewa katika wadhifa wake.

Gachagua aliwasili katika majengo ya Mahakama hiyo yaliyoko eneo la Milimani jijini Nairobi, akiwa na msafara wa magari sita akiambatana na Mbunge wa Embakasi ya Kati, Benjamin Gathiru, Cleophas Malala, maarufu kama Major Donk, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha United Democratic Alliance (UDA).

Katika kesi iliyofunguliwa na Ruto mahakamani hapo, alidai kwamba kesi zote zilizowasilishwa zinakiuka Kifungu 140 kama kinavyosomwa pamoja na vifungu vya 148 na 149 vya katiba, ambavyo vinaipa Mahakama ya Juu, mamlaka ya kuamua mizozo inayotokana na mchakato wa uchaguzi wa urais.



"Kwa mujibu wa Kifungu cha 165 (5) (a) cha Katiba, Mahakama hii haiwezi kuamua kesi na kutoa maagizo iliyoombwa, kwa kuwa ni suala ambalo limepewa Mahakama ya Juu," alidai Rais Ruto kupitia wakili wake Adrian Kamotho.

Gachagua na walalamikaji wengine kadhaa walipinga mchakato wa kumwondoa madarakani, kutokana na kutoshirikishwa Wakenya wengi na kushindwa kuthibitishwa kwa madai yote dhidi yake.

Jaji Chacha Mwita na Richard Mwongo, kutoka Mahakama Kuu ya Milimani na Mahakama Kuu ya Kerugoya, waliidhinisha kusikilizwa kwa kesi hizo kwa kueleza ni dharura na kuamua kusimamisha mchakato wa kujaza nafasi ya makamu rais.

Rais Ruto aliomba kesi hizo zitupiliwe mbali akidai kuwa zimewasilishwa kwa kunyume cha sheria na ni matumizi mabaya ya utaratibu wa kimahakama.

Wakili Kamotho alisema kesi hizo zinakiuka Ibara ya 143 (2) ya katiba na mamlaka ya wazi ya Mahakama ya Juu kwamba rais hawezi kushtakiwa akiwa uongozini kuhusiana na jambo lolote analofanya au kutofanya chini ya katiba.

"Kesi zilizoko hapa zina dosari isiyoweza kurekebishwa, inakiuka masharti ya sheria," alisema.

Kwa upande mwingine, wakati kesi ya Gachagua ikianza kusikilizwa hapo jana asubuhi, eneo la ndani na nje ya mahakama lilikuwa likilindwa vikali na polisi na maofisa wa usalama wakiwa na silaha. **Taifa leo**

# TANZANIA YAMALIZA FAINALI BSAFCON 2024 KWA VICHAPO

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Ufukweni imemaliza mechi za hatua ya makundi katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa mchezo huo (BSAFCON 2024) kwa huzuni baada ya juzi kupokea kichapo cha tatu.

Tanzania ilikubali kichapo cha mabao 10-3 dhidi ya Ghana, ikiwa ni mfululizo wa matokeo mabaya iliyokutana nayo katika fainali hizo zinazofanyika nchini Misri.

**Kikosi hicho cha Tanzania kilianza kwa kupoteza mchezo dhidi ya Morocco kwa kufungwa mabao 4-3 halafu ikachapwa mabao 9 -2.**

Kocha mchezaji wa timu hiyo, Jaruph Juma, alisema walijitahidi kadri ya uwezo wao kupambana lakini walizidiwa na wapinzani wao.

Juma alisema matokeo hayo yalichangiwa na ugumu wa kundi ambalo Tanzania ilipangwa katika fainali hizo.

"Lilikuwa ni kundi gumu sana, Morocco ni moja kati ya timu kubwa sana kwenye soka la ufukweni Afrika, Misri pia na hapo hapo ni wenyeji, nadhani kupoteza hizi mechi mbili ndiyo kumeondoa morali ya wachezaji katika mchezo wa mwisho kwa sababu hatukuwa na cha kutafuta," alisema kocha huyo.

Tanzania imeshika mkia kwenye kundi hiyo ikiwa haina pointi, huku wenyeji Misri wakiongoza kundi kwa pointi tisa, wakifuatiwa na Morocco waliomaliza na pointi sita.

Kundi B limeongozwa na Mauritania, waliomaliza wakiwa na pointi sita, sawa na Senegal ambayo nayo imetinga hatua ya mtoano.

Ghana iliyoshika nafasi ya tatu Kundi A, itacheza mshindi wa tatu wa Kundi B, Msumbiji katika mchezo wa 'play off'.

Hii ilikuwa ni mwaka wa tatu kwa Tanzania kushiriki fainali hizo.

# Mafunzo yaishusha Mwembe Makumbi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAFUNZO SC imetinga kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Wanajeshi wa Kipanga katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa juzi.

Matokeo hayo yameifanya Mafunzo kufikisha alama 16 alama sawa na Mwembe Makumbi City ambayo sasa iko katika nafasi ya pili.

Kocha Mkuu wa Mafunzo, Shekha Khamis, alisema mipango yake ya kushinda mechi zote hasa wanapokuwa nyumbani Unguja ipo pale pale.

**Mipango yake ya kushinda mechi zote hasa wanapokuwa nyumbani Unguja ipo pale pale.**

Khamis alisema amekiimarisha kikosi chake kucheza kwa umakini na kukusanya mapema pointi kutokana na kasi na ushindani uliopo katika Ligi Kuu Zanzibar.

Alisema katika mchezo huo timu yake ilitawala kipindi cha kwanza ambapo walifanikiwa kufunga mabao hayo mawili na Kipanga walitawala kipindi cha pili.

"Bado ligi ni ngumu sana, hakuna timu nyepesi kila mchezo unaoshuka uwanjani unaugumu wake, hata ukiangalia alama ambazo zipo kuanzia nafasi nne za juu utofauti wake labda alama mbili au moja , pia ni sawa na timu zilizo mkiani, hivyo tutaendelea na maandalizi kabambe kwa ajili ya kila mchezo," alisema Khamis.



Watoto wa Kituo cha Africarre wakionyesha umahiri katika sarakasi kwenye Tamasha la Tatu la Watoto lililoandaliwa kwa ajili ya kuonyesha kazi zao za sanaa na utamaduni lililofanyika Bagamoyo mkoani Pwani, juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Tamasha la watoto Bagamoyo lasifiwa

**Na Faustine Feliciane**

MRATIBU wa kupinga masuala ya Ukatili wa Jinsia kutoka Bagamoyo mkoani, Pwani, Monica Mgani, ameipongeza Taasisi ya Africare kwa kuandaa Tamasha la Watoto lenye lengo la kuwajenga kimaadili kwa njia ya sanaa na utamaduni, imeelezwa.

Tamasha hilo limehusisha watoto wa kuanzia umri wa miaka mitano hadi 15.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mgani alisema njia hiyo inachangia kutoa mafunzo kwa jamii kupitia kazi hizo za sanaa za watoto ili kupunguza hali ya ukatili wa kijinsia katika wilaya hiyo.

Mgani alisema utumiaji wa sanaa na utamaduni kwa watoto ni njia mojawapo ya kuwafikishia ujumbe ambao utawasaidia kujikita na matukio ya ukatili wa kijinsia.

"Nawapongeza kwa tamasha hili la tatu ambalo linaleta tija kwa jamii na kufikisha ujumbe wa aina mbalimbali kwa kutumia sanaa na utamaduni wa watoto katika kutatua changamoto zao, kupitia sanaa hizi ujumbe utafika na kuwasilishwa kwa wazazi ipasavyo ili kutokomeza ukatili wa kijinsia," Mgani alisema.

Aliongeza katika tamasha hilo, Mkurugenzi wa Taasisi ya Africarre, Anjela Ngowi, alisema huu ni mwaka wa nne tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo ila kwa tamasha lao linafanyika kwa mara ya tatu.

Alisema taasisi hiyo inajikita katika kuendeleza watoto kukuza vipaji vya sanaa na utamaduni kwa sababu asilimia kubwa ya shule wanazosoma hazina nafasi ya kujifunza sanaa na utamaduni.

"Taasisi yetu kwa kuona hivyo tukaona ni vizuri watoto wakawa wanapata elimu katika kituo chetu maana ni masomo ya sanaa na utamaduni," alisema mratibu huyo na kuongeza; " Masomo haya yanaweza kumpa mtoto uwezo wa kujitegemea, kujiamini na kujitambua kwa sababu watoto wanajifunza na kuelimisha jamii ana kwa ana kwa kujulisha umma kuwa maisha yao yanatakiwa yawe namna gani, ni kitu gani kinawakera katika maisha yao ya kila siku," Mgani alisisitiza.

Katika tamasha hilo, watoto walishiriki michezo mbalimbali kama sanaa za maonyesho, sarakasi na kuimba.

## ZISIKUPITE

### XAVI ATAJWA MAN UNITED

KOCHA wa zamani wa Barcelona, Xavi amefanya mazungumzo na Manchester United kuhusu uwezekano wa kuchukua nafasi ya Erik ten Hag. ***(Mail)***

### GRAY ATAKIWA KWA MKOPO

KLABU ya Sevilla ina nia ya kumsajili beki wa Tottenham Hotspur mwenye umri wa miaka 18, Archie Gray kwa mkopo. ***(Mucho Deporte)***

### ATAKIWA KUSAINI

CHELSEA imemwambia mlinzi wa umri wa miaka 18 wa England, Josh Acheampong kwamba hataichezea klabu hiyo kwa kiwango chochote tena hadi asaini mkataba mpya. ***(Athletic)***

### PEDRO PORRO AWEKEWA BEI

TOTTENHAM Hotspur imeweka bei ya pauni milioni 80 kwa beki wa Hispania, Pedro Porro mwenye umri wa miaka 25, ambaye anawindwa na Manchester City. ***(Football Insider)***

### ZYCH AZIVUTIA MBILI EPL

KLABU za Brighton na Arsenal zinavutiwa na kipa wa Aston Villa mwenye umri wa miaka 21 raia wa Poland, Oliwier Zych. ***(Telegraph)***

### WILSHERE RASMI NORWICH

KOCHA wa Arsenal kwa wachezaji vijana wenye umri wa chini ya miaka 18, Jack Wilshere mwenye umri wa miaka 32, atajiunga na Norwich kama kocha wa kikosi cha kwanza wiki hii baada ya klabu hizo mbili kukubaliana ada ya fidia kwa kiungo huyo wa zamani wa Washikabunduki. ***(Standard)***

### POTTER, MOYES WATAJWA

GRAHAM Potter, David Moyes na Gareth Southgate wanatarajiwa kurithi mikoba ya Oliver Glasner iwapo atatimuliwa na Crystal Palace. ***(Guardian)***

### TERZIC KUMRITHI JULEN

KOCHA wa zamani wa Borussia Dortmund, Edin Terzic atawania kazi katika klabu ya West Ham iwapo wagonga nyundo hao watamfukuza Julen Lopetegui. ***(Florian Plettenberg)***

### ATAKIWA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund inataka kumsajili beki dirisha la Januari huku mchezaji wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 27, Ben Chilwell na mchezaji wa kimataifa wa Hungary na Bournemouth, Milos Kerkez mwenye umri wa miaka 20, wakijumuishwa kwenye orodha yao fupi. ***(Team Talk)***

### EVERTON KUNUNULIWA

MPANGO wa Freidkin Group wa kuinunua klabu ya Everton unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, lakini wamiliki hao wapya hawataidhinisha matumizi makubwa ya Januari kwa sababu ya vikwazo. ***(The i)***

## DONDO… SOKA MAGAZ… ULAYA



# PULISIC AZUNGUMZIA BAO LAKE LA BAHATI

**MILAN,** Italia

**Nyota huyo wa Marekani alia na kufunga bao lake ambalo ameliita la...**

CHRISTIAN Pulisic aliendelea na mwanzo wake mzuri wa msimu Jumanne iliyopita baada ya kufunga moja kwa moja kutoka kwenye kona katika ushindi wa 3-1 wa AC Milan wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Club Brugge ya Ubelgiji.

**Nyota huyo wa Marekani alianza kufunga dakika ya 34 kwenye Uwanja wa San Siro, akitumia kona iliyopinda kutoka upande wa kushoto ambayo iliwahadaa kipa na mabeki na kuwapita kabla ya kutinga wavuni.**

Pulisic sasa amefikisha mchango wa mabao 10 katika michezo yake 10 iliyopita kwa klabu na nchi yake.

Lilikuwa pia bao la pili kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 katika mechi tatu za Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, baada ya kufunga katika mechi ya ufunguzi ya Milan dhidi ya Liverpool mwezi uliopita.

Baada ya bao la Jumanne, Pulisic aliinua mikono yake juu na kutabasamu kwa upana kabla ya kukumbatiwa na wachezaji wenzake, huku akicheka akionekana kutokuamini. Na baadaye alikubali bao hilo lilikuwa na kipengele cha bahati.

"Leo ilikuwa bahati kidogo lakini bado inafaa. Nina furaha sana kwa bao hili la bahati," alisema Pulisic.

"Sikujaribu kufanya hivyo lakini ilikuwa krosi nzuri, nitasema hivyo, baada ya bao zuri na lakini sikuwa nikijaribu kufanya hivyo mazoezini ndio maana nasema imekuwa bahati kidogo," alisema nyota huyo.

Katika Serie A, Pulisic amefunga mabao matano na kuongeza asisti tatu katika mechi nane za kampeni hii. Pia aliasisti katika mchezo wa kwanza wa Mauricio Pochettino kuinoa timu ya taifa ya Marekani dhidi ya Panama mapema mwezi huu.

"Ninafanya kazi kwa bidii kila siku. Siku zote nataka kuwa na uamuzi katika mechi," alisema.

"Nina furaha sana mwaka huu, ninapata mabao mengi na pasi za mabao, lakini sio hivyo kila wakati. Kwa hiyo nitaendelea hivi na nina matumaini ya kuendelea kufunga."

Brugge ya Ubelgiji ililazimika kucheza muda mwingi wa mchezo wa Jumanne ikiwa na wachezaji 10 baada ya Raphael Onyedika kutolewa nje kwa kadi nyekundu dakika ya 40 lakini bado walisawazisha bao la Kyriani Sabbe dakika ya 51.

Tijjani Reijnders baadaye alifunga mara mbili na kuipa Milan ushindi wa kwanza uliohitajika sana katika Ligi ya Mabingwa msimu huu, baada ya kufungwa na Bayer Leverkusen.

# ANCELOTTI: VINICIUS ANA NGUVU YA AJABU




**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti alisifu 'nguvu ya ajabu' ya Vinícius Júnior baada ya nyota huyo anayewania tuzo ya Ballon d'Or kufunga 'hat trick' katika ushindi wa mabao 5-2 wa Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Borussia Dortmund, juzi.

Madrid walitoka nyuma kwa mabao 2-0 wakati wa mapumziko katika dimba la Santiago Bernabeu baada ya Donyell Malen na Jamie Gittens kuwafungia wageni kabla ya mabao ya Antonio Rüdiger, Vinícius na Lucas Vázquez kuwaweka mbele mabingwa hao wa Ulaya.

Mchezaji wa kimataifa wa Brazil, Vinicius alifunga mabao mawili zaidi kukamilisha hat trick yake na kuwaacha Madrid wakiwa katika hali nzuri kabla ya mechi ya Jumamosi ya Clássico dhidi ya Barcelona.

"Si kawaida kwa mchezaji kuwa na kipindi cha pili kama alivyokuwa," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Alicheza kwa nguvu ya ajabu na hii isiyo ya kawaida."

'Hat trick' ya Vinicius ilikuja chini ya wiki moja kabla ya mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or ya 2024 kutangazwa katika hafla itakayofanyika jijini Paris.


"Nadhani Vinicius atashinda, lakini si kwa sababu ya kile alichokifanya usiku wa leo (juzi)," alisema Ancelotti.

"Itakuwa kwa sababu ya kile alichokifanya msimu uliopita. Mabao matatu usiku wa leo (juzi) yatamsaidia kushinda Ballon d'Or ijayo!"

"Tunajua kuwa nyumbani, na mashabiki wetu, chochote kinaweza kutokea," Vinicius aliiambia Movistar.

"Tulipofika kwenye chumba cha kubadilishia nguo wakati wa mapumziko tulikuwa kimya sana, tulimsikiliza bosi tu. Na alisema jambo moja, ikiwa tutafunga bao la kwanza, tutarudi mchezoni. Na tulifanya hivyo."

# Calafiori hatihati kuivaa Liverpool




**LONDON,** England

MIKEL Arteta anahofia kwamba Riccardo Calafiori anaweza kujiunga na orodha ya majeruhi wanaoongezeka ya Arsenal lakini akasema Washikabunduki hao watakuwa fiti dhidi ya Liverpool, Jumapili.

Calafiori alichechemea kutoka katika ushindi wa 1-0 wa Ligi ya Mabingwa Jumanne dhidi ya Shakhtar Donetsk Uwanja wa Emirates dakika 18 kabla ya kumalizika kwa mchezo, baada ya kuanguka vibaya.

Beki huyo wa Italia, aliyesajiliwa kwa pauni milioni 42 majira ya joto kutoka Bologna, atatathminiwa siku zijazo lakini Arteta alikiri kuwa dalili za awali hazikuwa na matumaini.

Arteta pia alisema hana uhakika kama Bukayo Saka atakuwapo kukabiliana na vinara wa Ligi Kuu ya England, Liverpool wikendi hii huku akipambana na tatizo la msuli wa paja huku Martin Ødegaard (kifundo cha mguu) na Jurriën Timber (maumivu ya misuli) pia ni mashaka makubwa.

Huku William Saliba akiwa amesimamishwa kufuatia kadi nyekundu huko Bournemouth, Arteta anaweza kuamua kumtumia kiungo Thomas Partey katika safu ya ulinzi baada ya kuonesha mchezo hafifu dhidi ya Shakhtar ambapo kipa Dmytro Riznyk alifunga bao la dakika ya 29 na kumaliza mchezo.

# Raphina afichua, Williams alimvuruga

**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Raphinha amesema aliumizwa na uvumi kuhusu nia ya klabu hiyo kutaka kumsajili Nico Williams msimu wa majira ya joto.

Kufuatilia kwa Barca kwa Athletic Club na winga wa Hispania kulizua maswali kuhusu mustakabali wa Raphinha, huku picha moja ya shabiki akiwa amevaa shati ya Williams yenye namba 11 ya Mbrazili huyo ikisambaa wakati wa dirisha la usajili.

Raphinha, ambaye baadaye ameanza msimu akiwa katika kiwango kizuri na jana Jumatano alitarajiwa kucheza mechi yake ya 100 kwa Barca dhidi ya Bayern Munich, amekiri kukerwa na mambo fulani wakati wa majira ya joto.

"Niliona machapisho hayo yakiwa na jezi kwenye Instagram," alisema katika mkutano na wanahabari.

"Nilidhani ulikuwa utani wa ladha mbaya na haukuwa na heshima.

"Watu wanahitaji kuheshimu wachezaji walioko hapa. Tuko hapa kujitolea kwa uwezo wetu wote na kupigania klabu. Kuona picha kama hiyo haikuwa nzuri kwangu, niliichukulia kama kunikosea heshima.

"Kwa kweli, watu wako huru kufanya wanachotaka, lakini nilihisi kuumia kidogo wakati huo."

Chini ya Kocha Hansi Flick, amepata kiwango bora zaidi tangu ajiunge na klabu hiyo akitokea Leeds United mwaka 2022, akifunga mabao sita na kutoa pasi za mabao sita katika mechi 12 alizocheza kwenye michuano yote.

Akicheza kutoka upande wa kushoto au zaidi katikati, kinyume na winga ya kulia, alichaguliwa Mchezaji Bora wa Mwezi wa LaLiga, Agosti.

Hata amekuwa akivaa kitambaa cha unahodha wakati fulani, lakini alisisitiza kuwa uvumi wa majira ya joto hauko nyuma ya kuimarika kwake.

"Haikuwa motisha ya kuongeza kuanza msimu kwa jinsi nilivyofanya," aliongeza.

"Nilikuwa na hamu ya kujitolea kwa uwezo wangu wote kwa ajili ya klabu. Kuona ni miaka mingapi ya mkataba wangu ninao hapa (hadi 2027), ilikuwa hatua muhimu.

## Gamondi atambia ubora wa Yanga

INATOKA UK. 24

tutaendelea kupambana kila idara ili kutimiza malengo yetu," Gamondi aliongeza.

Naye Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally, alisema timu yake ilipoteza utulivu na hali hiyo iliwapa nafasi wapinzani wao kupata mabao yaliyowapa ushindi. Ally alisema pia kadi nyekundu iliyotolewa na kipa wake chaguo la kwanza, Denis Richard, kuliwafanya wabadilishe mpango wa mechi hiyo ambao waliingia nao.

Hata hivyo anasema anasikitika kuona wachezaji wake wamepoteza nafasi mbili za wazi za kufunga mabao ambazo walitengeneza katika mchezo huo. Coastal Union ambao watakuwa wenyeji wa mchezo huo wamehamia Arusha kwa sababu uwanja wao wa asili wa CCM Mkwakwani ulioko jijini Tanga unafanyiwa ukarabati.

Mechi nyingine za Ligi Kuu Tanzania Bara zinatarajia kuchezwa kesho kwa Singida Black Stars kuwakaribisha Fountain Gate wakati Namungo itawafuata Simba na Azam FC itawaalika KenGold kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

## Fadlu: Kipa Prisons amepunguza

INATOKA UK. 24

kilikuwa ndiyo muhimu zaidi," alisema kocha huyo.

Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema haukuwa mchezo rahisi kwa sababu Prisons walikuwa bora katika kuzuia mashambulizi yao.

"Ili uifunge Prisons ni lazima wafanye makosa ndiyo uyatumie, jana (juzi), tulinufaika na makosa yao, tunasema haikuwa rahisi kushinda kulingana na ufinyu wa ratiba na wingi wa mechi mfululizo, pamoja na aina ya mpinzani tuliyecheza naye," alisema Ahmed.

Naye Kocha Mkuu wa Prisons, Mbwana Makata, alisema kama si kosa alilofanya Mbisa, basi matokeo yangekuwa tofauti.

"Udhaifu wa golikipa kudaka mpira ndiyo uliotugharimu, ila uimara katika ulinzi ulikuwa mzuri, Simba walishindwa kupata mianya, tukawa tunawanyima muda wa kuandaa mashambulizi, wakabadilika wakaanza kucheza mipira mirefu.

Nasema leo (juzi), timu iliimarika zaidi na kama isingekuwa makosa ya kipa, nadhani hadithi ingekuwa nyingine," alisema kocha huyo.

Simba sasa imefikisha pointi 16, ikishinda michezo mitano, sare moja na kupoteza mmoja, huku Prisons ikiwa katika nafasi ya 12 ikisalia na pointi saba kibindoni baada ya kushuka dimbani mara nane.

# CHE MALONE, BACCA VITANI LIGI KUU BARA 2024/2025

**Na Adam Fungamwango**

MBALI na timu kupigania ubingwa, kusaka kiatu cha dhahabu, kutoa pasi za mwisho, 'asisti' na hata 'clean sheets' kwa makipa, kumezuka vita nyingine ya mabeki wa kati wa Simba na Yanga, Che Malone Fondoh na Ibrahim Hamad 'Bacca', kushindana kufunga mabao katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, inayoendelea.

Bao la dakika ya nne alilofunga kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya juzi limemfanya beki wa Simba, raia wa Cameroon, Che Malone, kumfikia Bacca ambaye amefunga mabao mawili mpaka sasa kwenye ligi hiyo.

**Che Malone alitumia makosa ya kipa, Mussa Mbisa wa Prisons kushindwa kuukamata mpira vizuri, ukamponyoka na kuelekea langoni, licha ya juhudi zake za kuurukia na kutaka kudaka kushindikana, lakini mguu wa kushoto wa Che Malone ulifanikiwa kuukwamisha wavuni.**

Lilikuwa ni bao pekee katika mchezo huo likiipa Simba pointi tatu muhimu za ugenini dhidi ya Prisons, ambayo msimu uliopita iliondoka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Wekundi wa Msimbazi.

"Lengo lilikuwa kushinda mchezo, kazi yangu ni kulinda, lakini kuna wakati naenda kusaidia washambuliaji, siwezi kusema kama nafanya hivi peke yangu, soka ni kundi, ni mchezo wa watu wengi, hivyo na mimi nawapongeza wachezaji wenzangu kwa kuipambania timu.

Nimefunga, nimezuia, tumepata ushindi, nimekuwa mchezaji bora, siku zote timu kubwa haiwezi kupoteza mechi au pointi mara kwa mara, tulipoteza mchezo uliopita, lakini leo (juzi), tumesawazisha makosa," alisema beki huyo wakati akikabidhiwa tuzo ya mchezaji bora wa mechi hiyo.

Bao lake la kwanza alilifunga Agosti 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC, Dar es Salaam, alipopachika kwa kichwa dakika ya 13, akiiongoza Simba kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Tabora United.

Bacca, ambaye na yeye ana mabao mawili, alifunga Septemba 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya, Yanga ikiifunga Prisons bao 1-0, kabla ya Oktoba 3 kupachika goli lingine kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam dhidi ya Pamba, timu yake ikiondoka na ushindi wa mabao 4-0.

"Mwaka huu naingia rasmi katika kinyang'anyiro cha kusaka kiatu cha dhahabu, mastraika wote hata wa Yanga wajiandae," alisema Bacca.



Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema (mwenye fulana nyeupe), akiongoza mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na michezo ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayoendelea tena kuanzia Novemba 5, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

## *Mwambusi atua Coastal Union*

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa zamani wa Mbeya City, Ihefu na Yanga, Juma Mwambusi, ameanza kazi rasmi ya kuifundisha Coastal Union, klabu hiyo imethibitisha.

Mwambusi aliyehudumu kama Kocha Msaidizi wa Yanga chini ya Mholanzi, Hans van Pluijm, amesaini mkataba wa mwaka mmoja kuitumikia timu hiyo yenye maskani yake jijini Tanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa habari wa Coastal Union, Abass El Sabri, alisema uongozi una matumaini na kocha huyo kutokana na uzoefu wake katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Ni kweli tumemalizana na Kocha Mwambusi, ameanza kazi ya kukinoa kikosi chetu, tunaamini kwa uwezo wake na uzoefu wa Ligi Kuu, timu yetu ipo kwenye mikono salama na tunaweza kufanya vizuri," alisema Sabri.

Mwambusi amejiunga na Coastal Union akichukua mikoba iliyoachwa na David Ouma, ambaye alitimuliwa tangu Agosti mwaka huu kutokana na matokeo yasiyoridhisha.

Kocha huyo anaanza kibarua huku Coastal Union yenye pointi nane ikiwa kwenye nafasi ya tisa katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo vinara ni Singida Black Stars wenye pointi 19.

Michezo

Alhamisi Oktoba 24, 2024

Nipashe



Pulisic azungumzia bao lake UKURASA 21



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Clatous Chama (kushoto), akiwania mpira dhidi ya winga wa JKT Tanzania, Shiza Kichuya, katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi usiku. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# GAMONDI ATAMBIA UBORA WA YANGA

## Kocha huyo afunguka ndio unaamua matokeo ya mechi...

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya timu yake kuendelea kupata ushindi mfululizo katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema ubora wa wachezaji walioko katika kikosi chake ndio unaamua mechi.

**Ushindi wa mabao 2-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi uliifanya Yanga kutimiza michezo 22 bila kufungwa, katika mashindano yote waliyocheza.**

Matokeo hayo yaliwafanya mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kufikisha pointi 18 baada ya kucheza michezi sita na kupanda hadi nafasi ya pili huku vinara wakiwa ni Singida Black Stars yenye pointi 19, lakini wamecheza mchezo mmoja zaidi.

Simba yenye pointi 16 na imeshuka dimbani katika michezo saba iko kwenye nafasi ya tatu ikifuatiwa na Fountain Gate yenye pointi kama hizo, lakini imecheza mechi nane.

Akizungumza na gazeti hili jana, Gamondi, alisema timu yake imecheza mechi mbili ngumu mfululizo dhidi ya Simba na JKT Tanzania, lakini matokeo mazuri waliyapata yanatokana na ubora pamoja na viwango 'vikubwa' vya wachezaji wake.

Gamondi alisema anafurahishwa na viwango vinavyoonyeshwa na wachezaji wake katika kila mechi wanayoshuka uwanjani.

"Tumecheza mechi mbili ngumu, tulianza dhidi ya Simba na siku chache baadaye tunakutana na JKT ambayo ni timu ngumu, nashukuru wachezaji wamepambana na tumefanikiwa kupata ushindi," alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema katika mchezo huo wa juzi walifanikiwa kumiliki mpira na kutengeneza nafasi nyingi kipindi cha kwanza na kupelekea kupata mabao hayo mawili.

"Kipindi cha pili wapinzani wetu licha ya kuwa pungufu, walirudi uwanjani na nguvu kubwa, walicheza vizuri na kujaribu kutengeneza nafasi, lakini kama nilivyosema ubora wa wachezaji wangu umeamua mechi," alitamba Gamondi.

Kocha huyo raia wa Argentina alisema kwa sasa wanaelekeza nguvu yao katika mechi inayofuata ambapo watawafuata wenyeji Coastal Union kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

"Mechi hii imemalizika, sasa akili na mipango yetu tunaangalia mchezo unaofuata, hakuna mechi rahisi kwa sababu kila timu inahitaji kupata pointi,

INAENDELEA UKURASA 23

## Fadlu: Kipa wa Prisons amepunguza mabao yetu

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davis, amemtaja kipa wa Prisons, Mussa Mbisa, ndiye aliyewanyima ushindi mnono katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya juzi.

Simba ilipata ushindi wa bao 1-0 katika mechi hiyo, shukrani beki wa kati, Che Malone Fondoh, ambaye alimalizia mpira uliotemwa na Mbisa.

Hata hivyo, Mbisa ndiye aliyekuwa shujaa wa mchezo huo kwa kuokoa mashambulizi mbalimbali yaliyomlenga na kuifanya Simba kupata ushindi mwembamba katika mchezo huo.

Uimara wa kipa huyo uliokoa Simba kufunga mabao mengine mawili ya wazi katika mechi hiyo iliyochezeshwa na mwamuzi, Amina Kyando, kutoka mkoani Morogoro.

"Kilikuwa kiwango kizuri mno kwa kipa wao, alikuwa shujaa kwa sababu aliokoa hatari nyingi ambazo zingekuwa mabao, licha ya kufanya makosa na kupatikana bao, lakini huyo ndiye aliyesababisha wasipigwe nyingi," alisema Fadlu.

Kocha huyo raia wa Afrika Kusini alilalamika Uwanja wa Sokoine haukuwa katika ubora unaotakiwa hivyo kuwafanya wachezaji wake washindwe kuanzisha zaidi mashambulizi kutoka nyuma kwa kuhofia kupoteza kutokana na changamoto hiyo.

"Tumecheza mechi kwenye kiwanja ambacho hakikuwa vizuri, ilibidi kukimbizana na kusaka mpira inayodunda, Mohamed Hussein 'Tshabalala' na Kibu Denis wamekuwa wachovu kwa sababu wametoka kwenye kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), hawajapumzika na wamecheza kiasi cha michezo sita kwa muda mfupi tu," Fadlu alisema.

Aliongeza amefurahi kupata ushindi huo pamoja uliotokana na wachezaji wake kupambana.

"Ninachofurahi tumepata ushindi kwenye mchezo mgumu, tumecheza vizuri, tumetengeneza nafasi nyingi, nadhani hiki

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >